# Nipashe

Ijumaa Machi 12, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580517

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



BUFE

Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Bosi TPDC achambua uchumi gesi unavyokaribisha Tanzania Viwanda

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

Kiwanda rasmi cha kinamama wa Sengerema, kila kitu ni wao

• Mazao kuharibika 'stop', mifugo faida tupu

UKURASA 11

**Sanduku** lenye nyoka laibua kizaazaa sokoni

UKURASA 2



**Waziri:** Watumishi waliorejesha fedha wachukuliwe hatua

UKURASA 3



# Ukiwa na vitu hivi figo zako hatarini

• **Matibabu** yake mil. 40/-, wengi washindwa kumudu gharama... *Endelea ukurasa 2 na 16*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 4**

**WASHIKILIWA TUHUMA ZA KUSAFIRISHA VINYONGA NJE**

WATUHUMIWA watatu raia wa Tanzania wanashikiliwa kwa tuhuma za kushirikiana na raia...

**UKURASA WA 4**

**WABUNGE WATAKA FEDHA ZA MIRADI KUPELEKWA MAPEMA**

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), imeshauri Wizara ya Fedha...

**UKURASA WA 7**

**MAJALIWA ATOA SIKU 3 MALIPO YA WAKULIMA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameipa siku tatu kuanzia juzi kampuni ya DL iwasilishe maelezo ya kwanini hajawalipa wakulima...




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (kulia), akisalimiana kwa staili na Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, kabla ya kuwasilisha mapendekezo ya serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na kiwango cha ukomo wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2021/22, katika ukumbi wa Msekwa, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mpango aanika bajeti ya 6 serikali ya JPM

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# Mafao chanzo cha migogoro ya ndoa

UKURASA 2


**MICHEZO** **SIMBA SC: BADO TUKO VITANI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Sanduku lenye nyoka lazua kizaazaa sokoni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Mtaa wa Mwantengule katika Kata ya Isyesye jijini Mbeya, wamekumbwa na taharuki baada ya kuamka na kukuta sanduku lenye nyoka mkubwa aina ya chatu likiwa limetelekezwa sokoni na watu wasiojulikana.

Sanduku hilo linadaiwa kutelekezwa mahali huko majira ya saa saba usiku wa kuamkia jana na kugunduliwa na walinzi wa maduka yaliyoko kwenye eneo hilo.

Akizungumzia tukio hilo, mmoja wa walinzi hao, Galib Sanga, alisema kuwa baada ya kuliona sanduku hilo, waliamua kulilinda kwa muda, lakini baadaye wakashtuka na kuhisi huenda limeachwa hapo na wahalifu waliokuwa wameliiba mahali fulani na huenda ndani kuna mali.

"Sanduku hili tulipoliona lilikuwa limefungwa kwa kufuri, lakini baada ya kulistukia tuliamua kuvunja kufuri na ndipo tukalifunua na kukuta joka kubwa likiwa ndani yake," alisema Sanga.

Alisema walipomwona nyoka huyo, waliingiwa na hofu na kulifunika sanduku hilo wakaliacha mpaka asubuhi na ndipo wananchi wakaanza kujitokeza kwa wingi kumwangalia nyoka huyo.

Baadhi ya wananchi walioshuhudia tukio hilo, walilihusisha na imani za kishirikina wakidai siyo rahisi nyoka mkubwa namna hiyo kutoka msituni mwenyewe na kujiweka kwenye sanduku kisha akaonekana katika eneo hilo.

Mkazi wa eneo hilo, Lucy Mwambene, alisema haamini kwamba nyoka huyo ameonekana eneo hilo kwa bahati mbaya, bali ni mkakati wa watu wenye imani za kishirikina.

"Tukio hili limenishangaza na kunipa hofu maana hatuwezi kusema tukio hili ni la maliasili, bali tunajua kuna mbinu za kishirikina zinahusika, inawezekana hilo joka kuna mahali mtu ametoka nalo likamshinda au aliiba sanduku hili akidhani lina mali kumbe ni joka," alisema.

Baada ya wananchi hao kutoa taarifa za uwapo wa joka hilo kwenye maeneo yao, maofisa maliasili kutoka Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) walifika katika eneo hilo na kulichukua kwa ajili ya hatua zaidi.

Kiongozi wa maofisa hao, Eunice Mbilinyi, alisema jukumu la kumlinda mnyama huyo siyo la TFS, bali Mamlaka ya Uhifadhi wa Wanyamapori (TAWA), lakini kwa vile mamlaka hiyo haina maofisa wake jijini Mbeya, walilazimika kuchukua hatua. Alisema waliamua kumchukua nyoka huyo na kumpeleka katika hifadhi ndogo ya wanyamapori inayomilikiwa na Kanisa la Uinjilisti Mbalizi iliyoko eneo la Ifisi wilayani Mbeya kwa ajili ya kuhifadhiwa.

"Tumefika na kumwona nyoka huyu aina ya chatu japo wataalamu wa wanyamapori watatueleza zaidi, akiwa ni mzima, hivyo tunamchukua na kumpeleka kwenye zoo (hifadhi ndogo ya wanyamapori) ya Ifisi ambako tunadhani yatakuwa ni mazingira salama ya kumhifadhi," alisema Eunice.

Hata hivyo, kutokana na uwapo wa kundi kubwa la wananchi waliokuwa wanashangaa nyoka huyo, askari wa Jeshi la Polisi walifika kwa lengo la kulinda usalama.

Hilo siyo tukio la kwanza kutelekezwa vitu vya ajabu jijini Mbeya. Januari Mosi mwaka jana, wananchi walikuta jeneza ambalo lilikuwa tupu likiwa limetelekezwa katika Soko la Soweto jijini hapo.



Joka aina ya chatu, lililokuwa limetelekezwa ndani ya sanduku na watu wasiojulikana katika Soko la Isyesye vilabuni, jijini Mbeya usiku wa kuamkia jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ukiwa na vitu hivi, figo ziko hatarini

**Na Christina Mwakangale**

MADAKTARI Bingwa wamebainisha kuwa watu wenye uzito kupindukia na unene usioendana na kimo, wako kwenye hatari zaidi ya kupata ugonjwa wa figo.

Vilevile, wataalamu hao wa afya wamesema matumizi holela ya dawa za kutuliza maumivu na zisizothibitishwa, zikiwamo za kienyeji, ni chanzo cha ugonjwa huo.

Bingwa wa Magonjwa ya Figo kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Onesmo Kisanga, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Siku ya Figo Duniani.

Alisema watu hao ambao chanzo cha unene wao hutokana na kutofuata misingi ya lishe bora, ni rahisi kupata ugonjwa wa figo kuliko watu wenye magonjwa ya kisukari na presha.

"Uzito pekee unaweza ukaharibu figo bila presha wala kisukari. Yaani bila kuwa na ugonjwa wa kisukari, mtu anaweza kuwa na hatari kubwa ya kupata ugonjwa wa figo.

"Licha ya kisukari kuongoza kwa kuua figo duniani, ikifuatiwa na presha, ugonjwa wa figo ni ghali na unaumiza.

"Alhamisi ya pili ya mwezi Machi ya kila mwaka, tunaadhimisha Siku ya Figo ili ktuoa elimu. Ni ugonjwa ambao ni mgumu na wa gharama na ni tatizo, ila unatibika," alisema.

Dk. Kisanga alitoa wito kwa wananchi kufanya vipimo angalau mara moja kwa mwaka, akisisitiza kuwa inasaidia kufahamu iwapo kuna dalili za ugonjwa huo. Alisema dalili za ugonjwa huo huchelewa na kufanya mgonjwa kufikia kiwango cha asilimia 70 hadi 90 cha figo kuharibika bila kuona tofauti yoyote mwilini.

"Unapokuwa unaanza kupata tatizo, inabidi uanze kusafisha damu, lakini hata kama una tatizo la figo maisha yanaendelea," alifafanua.

Dk. Kisanga pia alisema asilimia 10 ya watu duniani wana tatizo sugu la figo na kwamba utafiti uliofanya Kaskazini Mashariki mwa Tanzania na Chama cha Madaktari wa Figo nchini, ulibainia asilimia 6.7 ya watu wana tatizo hilo.

Rais huyo wa Chama cha Madaktari wa Figo Tanzania, alisema uelewa mdogo ndiyo sababu kuu ya ugonjwa huo ambao hauchagui rika.

"Kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Kuishi Salama na Ugonjwa wa Figo'. Ukiwa na hatua ya kwanza hadi ya tatu, ugonjwa unatibika. Hatua ya nne na tano kuna magonjwa makubwa lakini maisha lazima yaendelee, utapatiwa dawa na tiba nyingine," alisema Dk. Kisanga.

Maadhimisho hayo jana yalikwenda sambamba na upimaji wa ugonjwa huo kwa watumishi takribani 500 wa MNH.

# Mafao chanzo migogoro ya ndoa

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

NDOA za wazee waliostaafu na kupata mafao pamoja na zile zenye miaka chini ya mitano zinaongoza kwa kuwa na migogoro mingi kuliko kundi lingine.

Kauli hiyo ilitolewa jana na mratibu wa kitengo cha kusuluhisha migogoro na kutetea haki za binadamu chini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini Magharibi, Naomi Kanyonyi, alipozungumza na Nipashe.

Kanyonyi alisema ndoa zenye umri mfupi chini ya miaka mitano zinaongoza kwa migogoro, pamoja na wazee waliostaafu na kupata mafao.

Akitaja sababu ya wastaafu kuongoza kwa migogoro alisema, wazee hasa wanaume wanapopata mafao, huongeza mambo ya anasa na kuwa na matumizi makubwa ya pesa ikiwamo kunywa pombe na kuleta kutoelewana kwa wanandoa.

Pia alisema wengine wanapopata mafao huongeza idadi ya wake kwa kuoa wanawake zaidi ya mmoja.

Alisema kwa mwaka 2020 walipokea migogoro 797 na kati ya hiyo 351 ni ya ndoa, ikifuatiwa na ya ardhi ambayo ni 200, ukatili majumbani 136, urithi 70 na 28 inahusu uchawi na ushirikina.

"Takwimu hizi zinathibitisha kuwa ukatili upo katika jamii na wanaoongoza kufanyiwa ukatili ni kinamama na watoto, hata kinababa wanafanyiwa, lakini kulingana na mila na desturi za kiafrika mara nyingi hawaripoti," alisema.

Alisema tangu mwaka 2004 kitengo hicho kilipoanzishwa walipokea mgogoro mmoja wa mwanaume aliyepigwa na mke wake, lakini migogoro mingi ya wanaume kupigwa na wake zao ipo, tena katika rika zote.

Kuhusu ukatili wa kijinsia majumbani, alisema inahusu wanaume kutelekeza wake zao na watoto.

Alitaja baadhi ya vyanzo vya migogoro ya ndoa kuwa ni kutopata mafundisho ya kutosha kabla ya kuingia kwenye ndoa na wanandoa wa sasa kukutana mitandaoni na kuoana bila kufahamiana kitabia.

"Ndoa za zamani wana ukoo, wanafamilia na wazazi walishiriki kumtafuta binti au kijana wa kiume kutoka katika familia ambazo wanaridhika nazo kitabia, lakini ndoa za siku hizi watu hawahusishwi wanaonana wawili baadaye utasikia wameoana," alisema.

Alisema ili kupunguza migogoro katika jamii hasa ya ndoa, wanawake wanatakiwa kuwafunda watoto wao kabla ya ndoa.

"Wanandoa wengi wanakwenda na mawazo ya kuwa ndoa ni kulala tu kitandani kumbe kuna zaidi ya hayo, hawajui kama kuna masuala ya kiuchumi, kulea watoto na mengine, hayo yote wakikutana nayo inakuwa ni changamoto na kusababisha ndoa kuingia katika mgogoro na hatimaye kuvunjika," alisema.

# Dk. Gwajima aagiza watumishi waliorejesha fedha washtakiwe

**Na Thobias Mwanakatwe,** SONGWE

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ameagiza watumishi wa afya mkoani hapa walioiba dawa za Sh. milioni 13.5 na kurudisha Sh. milioni 10.6, wafikishwe kwenye vyombo vya sheria.

Dk. Gwajima alitoa maelekezo hayo jana ikiwa muda mfupi baada ya kupokea taarifa ya Mkoa wa Songwe kuhusu huduma za afya akiwa katika ziara ya kikazi ya siku moja kwa lengo la kukagua ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa pamoja na utolewaji wa huduma za afya.

Pia aliwaagiza wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa nchini kuhakikisha wanazisimamia hospitali za mikoa ili kuleta uwajibikaji wa pamoja isipokuwa kwenye masuala ya kisheria.

"Vyombo vyote vya kisheria sasa vitahusika na vita dhidi ya wabadhirifu wa bidhaa za dawa, polisi, mahakama na TAKUKUTU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa)," alisema.

Akitoa taarifa ya mkoa kuhusu utoaji huduma za afya, Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe, Dk. Seif Shekalaghe, alisema moja ya changamoto zinazokwamisha ufanisi wa kiutendaji katika hospitali za mikoa na kuondoa dhana ya uwajibikaji wa pamoja ni kutokuwapo muundo mzuri unaowezesha wakuu wa mikoa na makatibu tawala kuwajibika kwenye shughuli zinazohusu hospitali hizo.

Dk. Shekhalaghe aliongeza kuwa hali hiyo imekuwa ikisababisha mkanganyiko mkubwa kwa kuwa imefika wakati wakuu wa mikoa wananyimwa taarifa zinazohusu hospitali hizo.

Akijibu changamoto hiyo, Dk. Gwajima alisema tayari wizara yake ilishatoa maelekezo ya namna ya utendaji wa pamoja kati ya menejimenti za hospitali za mikoa na wakuu wa mikoa na makatibu tawala. "Haiwezekani Mkuu wa Mkoa ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa asijue kitu chochote kinachofanyika katika hospitali ya mkoa wakati huko kuna rasilimali nyingi za serikali zimewekwa. Hili ni jambo la kushangaza sana," alisema.

"Wewe Katibu Tawala ndiye mkuu wa idara ya umma, hivyo unao wajibu mkubwa wa kusimamia hizi hospitali hasa kwenye eneo la rasilimali watu ili kuhakikisha nidhamu ya utendaji inakuwapo na kuleta tija," alisisitiza.

Dk. Gwajima alisema kuanzia Julai Mosi, mwaka huu, wizara itaanza utekelezaji mpango mpya wa kufuatilia na kupima tija na uwezo wa watendaji katika sekta ya afya nchini.

Alisema lengo la mpango huo ni kutaka sekta ya afya kuwa na watumishi wenye uwezo mkubwa wa kutoa huduma za afya na kuleta tija kwa wananchi, ikiwamo kuwaondoa watendaji wazembe na ambao wameshindwa kubadilika.

# Mpango aanika bajeti ya sita ya JPM

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (pichani), ameanika bajeti ya sita ya serikali ya awamu ya tano ambayo katika mwaka wa fedha wa 2021/22 inatarajia kuwa Sh. trilioni 36.3 ikiwa ongezeko la asilimia nne ya ile ya 2020/21.

Akiwasilisha Bungeni jana mapendekezo ya serikali ya mpango wa maendeleo wa taifa na kiwango cha ukomo wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2021/22, alisema makadirio hayo ya makusanyo ya fedha yamezingatia sera, misingi na vigezo vya ukomo wa bajeti.

Kati ya mapato hayo, Dk. Mpango alisema mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa Sh. trilioni 26 sawa na asilimia 71.8 ya bajeti yote, misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo Sh. trilioni 2.9, mikopo ya ndani Sh. trilioni tano na mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara Sh. trilioni 2.4.

"Katika mwaka 2021/22, serikali inapanga kutumia Sh. trilioni 36.3 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo, kati ya fedha hizo, Sh. trilioni 23 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikiwa ni asilimia 63 ya bajeti yote na Sh. trilioni 13.3 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, sawa na asilimia 37," alisema.

Pia alisema bajeti ya maendeleo inajumuisha Sh. trilioni 10 fedha za ndani, sawa na asilimia 78.2 ya bajeti ya maendeleo na Sh. trilioni 2.9 fedha za nje, ambazo ni asilimia 21.8.

Alisema Sh. trilioni 10.7 sawa na asilimia 29.5 ya bajeti yote zimetengwa kwa ajili ya kulipa fedha zilizokopwa kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo imekamilika na inayoendelea.

"Fedha hizo zilitengwa kwenye kasma za matumizi ya kawaida, lakini kimsingi si za kulipa mishahara wala posho," alisema.

Dk. Mpango aliainisha mchanganuo wa mapendekezo ya kiwango cha ukomo wa bajeti ya serikali kuwa ni mapato ya ndani kwa Serikali Kuu Sh. milioni 25,168,718, mapato ya kodi (TRA) Sh. 22,097,676, mapato yasiyo ya kodi Sh. 3,071,042, mapato ya Halmashauri Sh. milioni 863,858, misaada na mikopo nafuu kutoka washirika wa maendeleo Sh. 2,884,990.

Mapendekezo mengine ya bajeti ni misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya miradi Sh. 2,602,684, misaada na mikopo nafuu ya kisekta Sh. milioni 282,306, mikopo ya ndani na nje Sh. 7,341,240, mikopo ya nje Sh. 2,352,107, mikopo ya ndani Sh. 1,838,796, mikopo ya ndani-Rollover Sh. 3,150,337.

Kwa upande wa matumizi, alisema matumizi ya kawaida ni Sh. 23,002,951, mfuko mkuu wa serikali Sh. 10,663,278, malipo ya riba ndani Sh. 1,561,637 malipo ya mtaji ndani (Rollover) Sh. 3,150,337, malipo ya mtaji nje



Sh. 3,015,070, malipo ya riba nje Sh. 1,151,376, michango ya serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii Sh. 1,247,149, matumizi mengine ya Mfuko Mkuu Sh. 537,710 na mishahara Sh. 8,150,509.

Matumizi mengineyo ni Sh. 3,944,164, malipo ya madeni yaliyohakikiwa Sh. milioni 200,000, matumizi ya halmashauri (own source) Sh. milioni 532,768, matumizi mengineyo Sh. 3,211,396, mahitaji ya TANAPA, NCAA na TAWA Sh. milioni 245,000.

Katika mchanganuo wa matumizi hayo, matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa Sh. 13,255,855 ambapo fedha za ndani ni Sh. 10,370,865, malipo ya madeni yaliyohakikiwa Sh. milioni 400,000, reli ya kisasa (SGR) Sh. 1,174,246, mradi wa umeme wa Julius Nyerere Sh. 1,440,000, matumizi ya halmashauri Sh. milioni 331,090, miradi mingine Sh. 7,025,529, fedha za nje Sh. 2,884,990.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, serikali itaendelea kutekeleza hatua mbalimbali za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi, kugharamia mahitaji yasiyoepukika kama vile ugharamiaji wa miradi ya kipaumbele na kimkakati, deni la serikali, mishahara ya watumishi, mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, elimu msingi bila ada na uendeshaji wa ofisi," alisema.

Pia alisema serikali itaendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410.

"Lengo ni kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kuziba mianya ya uvujaji wa fedha za umma, vilevile serikali itaendelea kuhakiki, kulipa na kuzuia ongezeko la malimbikizo ya madai kwa serikali," alisema.

Alisema pia, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 pamoja na Bajeti ya mwaka 2021/22, unatarajiwa kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, upatikanaji wa huduma za kijamii, kuongeza fursa za ajira na maendeleo ya watu na nchi kwa ujumla.


SAO HILL AGRICULTURE LIMITED

REG: 86473

EXTRACT FROM THE MINUTES OF THE EXTRA - ORDINARY GENERAL MEETING OF SAO HILL AGRICULTURE LIMITED HELD AT ITS REGISTERED OFFICE

ON 15 DECEMBER 2020 AT 2:00 P.M.

**MEMBERS PRESENT WERE:**

| | |
|---|---|
| 1. GODLISTEN MINJA | DIRECTOR/ CHAIRMAN |
| 2. CHARLES SCOTT | DIRECTOR |
| 3. DANIEL HULLS | DIRECTOR |
| 4. PETER MACSPORRAN | DIRECTOR |
| 5. ANNETTE KIRETHI | COMPANY SECRETARY |

**THE CHAIRMAN REPORTED** that according to the Company activities, the Shareholders of **SAO HILL AGRICULTURE LTD** (hereinafter called "the Company") is desirous of voluntarily winding up the Company.

SPECIAL RESOLUTIONS:

**IT WAS RESOLVED.**

1. That, the Company be voluntarily liquidated and dissolved as decided by members;
2. That, Godfrey Basil Mramba be and is hereby appointed as a liquidator for the purpose of winding up the affairs and distributing the assets of the Company.
3. That, the remuneration payable by the Company to shall be negotiated and agreed based on the man-hour spent on this assignment;
4. That **M/S Basil & Alred** be and is hereby appointed auditor for the purpose of auditing the Liquidator's account of the winding up of the affairs of the Company;
5. That the remuneration payable by the Company to **M/S Basil & Alred** as auditor shall be negotiated and agreed based on the man-hour spent on this assignment.

The above is a certified True Copy of
The Resolution of the Board of Directors

CHAIRMAN COMPANY SECRETARY

TANGA FORESTS LIMITED

REG: 54988

EXTRACT FROM THE MINUTES OF THE EXTRA - ORDINARY GENERAL MEETING OF TANGA FORESTS LIMITED HELD AT ITS REGISTERED OFFICE
ON 15 DECEMBER 2020 AT 2:00 P. BOARD OF RESOLUTION

**MEMBERS PRESENT WERE:**

| | |
|---|---|
| 1. GODLISTEN MINJA | DIRECTOR/ CHAIRMAN |
| 2. LILIAN KITOSY | DIRECTOR /MEMBER |
| 3. ANNETTE KIRETHI | COMPANY SECRETARY |

**THE CHAIRMAN REPORTED** that according to the Company activities, the Shareholders of **TANGA FORESTS LIMITED** (hereinafter called "the Company") is desirous of voluntarily winding up the Company.

SPECIAL RESOLUTIONS:

**IT WAS RESOLVED.**

1. That the Company be voluntarily liquidated and dissolved as decided by members;
2. That Godfrey Basil Mramba be and is hereby appointed as a liquidator for the purpose of winding up the affairs and distributing the assets of the Company;
3. That the remuneration payable by the Company to shall be negotiated and agreed based on the man-hour spent on this assignment;
4. That **M/S Basil & Alred** be and is hereby appointed auditor for the purpose of auditing the Liquidator's account of the winding up of the affairs of the Company;
5. That the remuneration payable by the Company to **M/S Basil & Alred** as auditor shall be negotiated and agreed based on the man-hour spent on this assignment.

The above is a certified True Copy of
The Resolution of the Board of Directors

CHAIRMAN COMPANY SECRETARY

# Washikiliwa tuhuma za kusafirisha vinyonga nje

**Na Mwandishi Wetu**

WATUHUMIWA watatu raia wa Tanzania wanashikiliwa kwa tuhuma za kushirikiana na raia wa Jamhuri wa Czeck kusafirisha nje vinyonga 74 na nyoka 6 kinyume na sheria.

Akizungumza na vyombo vya habari leo mkoani Iringa, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amesema vinyonga na nyoka hao walikamatwa na maofisa wa forodha wa Austria wakiwa kwenye begi ambalo ndani yake waliwekwa kwenye soksi na kuingizwa kwenye vifungashio (container) vya plastiki.

Alisema watuhumiwa hao wanatarajiwa kufikishwa mahakamani leo kwa mashtaka ya makosa ya kusafirisha nje wanyamapori hao bila kibali, uhujumu uchumi na utakatishaji fedha kupitia biashara hiyo.

Dk. Ndumbaro alisema vinyonga na nyoka hao ambao waliokamatwa katika Uwanja wa Ndege wa Vienna nchini Austria, inadaiwa wametoka Tanzania katika Milima ya Usambara ambako kuna aina mbalimbali za vinyonga.

Akizungumzia jinsi watuhumiwa hao walivyowanaswa, Waziri Ndumbaro alisema baada ya kupata taarifa kupitia mitandao ya kijamii, wizara kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama na kwa kutumia Kikosi Kazi Taifa Dhidi Ujangili iliunda Kikosi Maalum cha kuchunguza tukio hilo.

Alisema kupitia taarifa za kiintelijensia, Kikosi Maalum kilifanikiwa kupata jina la mtuhumiwa aliyesafirisha vinyonga hao ambaye ni raia wa Jamhuri ya Czeck.

Hata hivyo, alisema uchunguzi unaendelea sehemu mbalimbali pamoja na kubaini namna vinyonga na nyoka hao walivyopitishwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) bila kugundulika.

Alisema watuhumiwa watakaobainika kuhusika na ujangili huo, watounganishwa na wenzao ambao wamekamatwa.

Waziri Ndumbaro alisema Serikali ya Tanzania itashirikiana na Austria katika uchunguzi unaoendelea ikiwamo kuwarudisha Tanzania vinyonga na nyoka hao.

Aidha, alisema serikali itawasiliana na Jamhuri ya Czeck ili watuhumiwa hao ambao ni raia wake wachukuliwe hatua.

Katika hatua nyingine, Waziri Ndumbaro amesema serikali inakusudia kuifuta kabisa biashara ya wanyamapori hai, ambayo ilizuiwa tangu Mei, 2016.

Amesisitiza kuwa hakuna mtu yeyote anayeruhusiwa kufanya biashara ya wanyamapori hai ndani na nje ya nchi na kwamba atakayebainika kufanya biashara hiyo, atachukuliwa hatua kali za kisheria.

## Akutwa na laini 74 zikiwamo 18 zenye usajili jina la mtu mmoja

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linawashikilia watu 23 kwa tuhuma za kuhusika katika matukio mbalimbali ikiwamo ya kukutwa na laini 74 zikiwamo 18 zilizosajiliwa kwa jina moja.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alibainisha hayo jana akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu kukamatwa kwa watu kwa tuhuma mbalimbali katika operesheni zilizofanyika katika wilaya tano za kipolisi za mkoa.

Kamanda Wankyo alisema watuhumiwa hao walikamatwa na vitu mbalimbali vikiwamo miche ya bangi, mirungi bunda 35, televisheni tatu, simu za mkononi tano, redio mbili, deki, king'amuzi na mashine ya kusajilia laini.

Alitaja vitu vingine vilivyokamatwa kuwa ni makoti 12 ya kampuni ya ulinzi SGA na laini 74 kati ya hizo 56 ni mpya na 18 zinazodaiwa kutumika kufanya utapeli zikiwa zimesajiliwa kwa jina moja la Moses Cosmas.

Kamanda huyo alisema idadi kubwa ya watuhumiwa wametoka katika Wilaya ya Kipolisi ya Mlandizi na majina yao yamehifadhiwa kwa sababu za kiusalama akiwamo anayemiliki laini zenye usajili wa jina la Moses Cosmas.

Pia alisema simu na televisheni viliibwa Mlandizi na kwamba watuhumiwa waliingia kwenye nyumba iliyokuwa na msiba na kupulizia dawa ya usingizi ambayo iliwafanya wafiwa wasishtuke na wakaiba vitu hivyo na kutokomea navyo hadi walipokamatwa katika msako huo.

Wanko alisema upelelezi kuhusiana na matukio hayo unaendelea na watuhumiwa watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma hizo.



Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Ofisa Teknolojia Maabara wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Musa Suko (kushoto), kuhusu mashine ya kupandikiza uroto, alipotembelea hospitali hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wabunge wataka fedha za miradi kupelekwa mapema

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), imeshauri Wizara ya Fedha na Mipango, kuhakikisha inawasilisha mapema fedha katika halmashauri ili kutekeleza miradi ya maendeleo iliyokusudiwa.

Aidha, imeziomba halmashauri kutumia vizuri fedha na kodi za wananchi kwa kuzielekeza kwenye mipango ya matumizi yaliyokusudiwa kwenye maeneo yao.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Grace Tendega, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mafunzo yanayotolewa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa kamati hiyo.

Alishauri, wizara kuhakikisha inawasilisha mapema fedha za miradi ya maendeleo kwenye halmashauri mbalimbali ili kukamilishwa miradi iliyokusudiwa.

Alibainisha kuwa kuna baadhi ya miradi ya maendeleo kwenye halmashauri inayokwama kukamilika kwa wakati, kutokana na kucheleweshwa kwa fedha za maendeleo kwenye halmashauri kutoka Hazina.

Alitaja sababu zingine za kucheleweshwa kwa fedha hizo ni kuchukua muda mrefu kutolewa kwa hundi kwa mkandarasi husika wa mradi na kucheleweshwa kwa mchanganuo wa miradi.

Kuhusu mafunzo, alisema lengo la ofisi ya CAG ni kuwajengea uwezo wajumbe wa kamati hiyo ili kutekeleza majukumu yao kikamilifu watakapozitembelea halmashauri.

Aliyataja baadhi ya majukumu ya kamati hiyo ni kuishauri serikali kuhusu utekelezaji wa miradi inayotekelezwa kwenye halmashauri ili kubaini sababu kwa baadhi ya miradi au kucheleweshwa.

Alitaja majukumu mengine ni kukagua miradi yote ya maendeleo ya halmashauri ili kubaini kama imejengwa kutokana na thamani ya fedha zilizotolewa na serikali.

Alisema mafunzo hayo yanawasaidia kujua namna ya kufuatilia fedha za umma zilizopelekwa halamashauri pamoja na kujua fedha ilivyotoka Hazina hadi kufika maeneo husika.

Hata hivyo, alisema kuna baadhi ya wataalamu wa halmashauri wemekuwa wakichelewesha mchangao wa mradi na kusababisha fedha kurudishwa tena Hazina

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Seleman Zedi, alisema mafunzo hayo yalianza Jumatatu ya wiki hii na yanatarajiwa kufanyika kwa kwa siku tatu na baada ya hapo kamati hiyo itaelekea kufanya mafunzo kwa vitendo kwenye baadhi ya halmashauri.

Alisema kamati itaelekea mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga kwa ajili ya mafunzo ya vitendo kwa kuitembelea baadhi ya miradi ya maendeleo iliyopo kwenye halmashauri.

HABARI KITAIFA




Waziri wa Madini, Doto Biteko, akikata utepe kuzindua kitabu cha mwongozi wa namna bora ya kuchukua sampuli kwa ajili ya uchunguzi wa madini katika maabara na mafunzo kwa viongozi wa shirikisho la vyama vya wachimbaji wa madini nchini, jijini Dodoma jana. **PICHA: MAELEZO**

# Mbaroni tuhuma utekaji raia wa China

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani Arusha, linawashikilia watu wawili akiwamo raia wa China kwa tuhuma za kumteka raia mmoja wa China, Mkazi wa Arusha na kumpeleka kusikojulikana ili kushinikiza wapewe dola za Kimarekani 100,000.

Aidha, watuhumiwa hao walikuwa wakishinikiza kupatiwa fedha hizo ili wamwachie huru.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alisema jana kuwa taarifa za kutekwa raia huyo wa China, ilitoka kwa raia mwenzake aliyetambuliwa kwa jina la Lian Qiang (44).

Alisema Machi 7, mwaka huu, Jeshi la Polisi lilipokea taarifa kutoka kwa Qiang kuwa mfanyakazi mwenzake wa kampuni ya Bonanza (jina limehifadhiwa) ambaye ni raia wa China, ametoweka katika mazingira ya kutatanisha.

Kwa mujibu wa Kamanda Masejo, raia huyo wa China alitoweka katika mazingira ya kutatanisha akiwa kikazi wilayani Karatu akiwa pamoja na dereva wakitumia gari aina ya Toyota Kluger lenye namba za usajili T.571 DLQ.

Alisema Qiang alipokea ujumbe wa kutakiwa kutuma dola 100,000 kwa watekaji ili mhusika aachiwe huru.

Kamanda Masejo alisema katika taarifa yake hiyo, Jeshi la Polisi lilichukua hatua za haraka na upelelezi ulibaini kwamba ametekwa na watu wawili, mmoja wao ni raia wa China na alikuwa mtumishi wa kampuni ya Bonanza ambaye alifukuzwa kazi kutokana na utovu wa nidhamu. Alisema watuhumiwa hao majina yamehifadhiwa kwa sababu za upelelezi.

Pia alisema watuhumiwa hao walikutwa katika nyumba ya kulala wageni iliyoko eneo la Ada Estate wilayani Kinondoni, Dar es Salaam pamoja na mateka ambaye alikuwa amefungwa kamba mikononi na miguuni.

Baada ya kukamatwa kwa watuhumiwa hao, alisema ulifanyika upekuzi na watuhumiwa walikutwa na gari aina ya Toyota Kluger lenye namba za usajili T. 982 DQA rangi ya Silver mali ya kampuni hiyo ya Bonanza lililoibiwa Arusha Februari 8, mwaka huu.

Mbali na gari hilo, alisema pia walikutwa na vitu mbalimbali ambavyo ni visu viwili, nyundo moja, mashine ya kuchorongea vitu (Drilling Machine) moja na Power Cable tano mali za Bonanza. Vitu vingine walivyokutwa navyo gari aina ya Kluger walilotumia kusafiria kutoka Arusha kwenda Dar es Salaam lenye namba za usajili T. 571 DLQ ambalo lilitelekezwa maeneo ya Clock Tower karibu na eneo la Benki ya Exim, jijini Dar es Salaam.

Kamanda alisema baada ya upelelezi kukamilika, jalada litapelekwa ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa hatua zaidi za kisheria.

# Serikali yageukia uvuvi maji asili

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema serikali imeweka lengo la kuhakikisha sekta ya uvuvi kupitia ufugaji samaki inazalisha samaki wengi hasa wanaopatikana kwenye vyanzo vya maji vya asili.

Akizungumza jana alipokagua shughuli zinazofanywa na Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji cha Kingolwira mkoani Morogoro, Waziri Ndaki alisema sekta ya ufugaji samaki imekuwa na mwitikio mkubwa kwa sasa kutokana na mahitaji ya soko lake kuongezeka.

Alisema wizara itahakikisha inaendelea kuboresha miundombinu ya uzalishaji vifaranga vya samaki na kupanua zaidi wigo wa uzalishaji wake ili viende sambamba na mahitaji ya vifaranga kwa watu wanaofuga samaki.

Naye Mkurugenzi wa Ukuzaji Viumbe Maji kutoka wizara hiyo, Dk. Nazael Madalla, alisema wako katika hatua mbalimbali za kuendelea kutoa elimu kuhusu ufugaji wa samaki ikiwamo kwa kutumia simu za mkononi.

Dk. Madalla alisema kupitia uboreshaji unaofanyika katika Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji cha Kingolwira, wako mbioni kuanza uzalishaji wa vifaranga vya samaki aina Kambale.

Pia alisema kwa sasa vituo vya ukuzaji viumbe maji vilivyo chini ya wizara hiyo vimeanza kuuza vifaranga aina ya sangara.

Kaimu Ofisa Mfawidhi wa Kituo hicho, Hamady Makorwa, alisema mkakati wao ni kuendeleza shughuli za uzalishaji ili kufikia lengo la kuzalisha vifaranga 600,000 kwa mwezi.

Alisema ili kufikia lengo hilo, kituo kinahitaji mabwawa 26 na samaki aina ya sato kwa ajili ya kuzalisha vifaranga 24,000 ambao kwa sasa wamefikia 5,430.


**SAO HILL AGRICULTURE LIMITED**

The companies Act, 2002 (Section 334)

**MEMBER'S VOLUNTARY WINDING – UP**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN** to the general public that **SAO HILL AGRICULTURE LIMITED** a company with registration number **86473** dully convened a meeting on 15th December, 2020 and passed a special resolution in accordance to section 333 (1) (b) of the Companies Act, 2002 that the company be wound up voluntarily.

All parties concerned and who have claims are hereby notified to submit their claims in a closed envelop within 30 days to **GODFREY BASIL MRAMBA of Basil & Alred, Ace Building, Haile Selassie Road, P.O. Box 78661, Dar es salaam, Tanzania**, who is appointed Liquidator of the Company.

**Any claims lodged after 30 days from this publication will not be considered for admission.**

**GODFREY BASIL MRAMBA**
**Liquidator**
**For SAO HILL AGRICULTURE LIMITED**

**TANGA FORESTS LIMITED**

The companies Act, 2002 (Section 334)

**MEMBER'S VOLUNTARY WINDING – UP**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN** to the general public that **TANGA FORESTS LIMITED** a company with registration number **54988** dully convened a meeting on 15th December, 2020 and passed a special resolution in accordance to section 333 (1) (b) of the Companies Act, 2002 that the company be wound up voluntarily.

All parties concerned and who have claims are hereby notified to submit their claims in a closed envelop within 30 days to **GODFREY BASIL MRAMBA of Basil & Alred, Ace Building, Haile Selassie Road, P.O. Box 78661, Dar es salaam, Tanzania**, who is appointed Liquidator of the Company.

**Any claims lodged after 30 days from this publication will not be considered for admission.**

**GODFREY BASIL MRAMBA**
**Liquidator**
**For TANGA FORESTS LIMITED**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ajira za madereva muhimu, kuwajali kwenye stahiki zao

**JUZI** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge, Ajira, Kazi, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, aliwaonya waajiri nchini kuendelea kuwatumia madereva kufanya kazi bila kuwa na mikataba rasmi.

Alionyesha kukerwa na kitendo hicho wakati wa kikao cha majadiliano kuhusu kero za madereva katika sekta ya usafirishaji.

Alisema sekta hiyo ni moja ya maeneo muhimu katika ukuaji wa uchumi, kwa kuwa isipokuwa na utulivu, uchumi wa nchi hautakuwa kutokana na madereva kuwa wahusika katika usafirishaji bidhaa na wafanyabiashara.

Suala la mikataba kwa kundi hili ni kilio cha muda mrefu na imekuwa ni kawaida kwa mtu kuwa na dereva kibarua nyumbani kwake, ofisini, kampuni na taasisi za binafsi.

Pamoja na mikataba rasmi, lakini kuna suala la mahitaji ya msingi ya madereva na stahiki zao nyingine, kutopewa msukumo kiasi cha wengi kuumia.

Madereva ni muhimu sana kwa kuwa wanabeba mustakabali wa anayeendeshwa, lakini wanaonekana siyo muhimu na kupewa ujira mdogo au wakati mwingine hauhesabiki kuwa ni ujira bali posho ya kuwawezesha kuishi.

Baadhi huwasahau kabisa hata kwenye mahitaji ya msingi kama ya chakula, unakuta bosi anakwenda baa au kwenye sherehe usiku dereva anakaa kwenye gari kumsubiri hadi usiku tena bila kula chochote.

Hakuna ubishi dereva huyo anakuwa hana mshahara na hata kama upo ni mdogo ambao hawezi kuugawa na kujinunulia cha ziada zaidi ya kuingia kwenye kutunza familia, na hata anaposafiri wakati mwingine ni rahisi kukopwa posho ya safari, lakini ya bosi ikapatikana.

Wakati mwingine bosi anasafiri na kusimama kwenye hoteli kubwa kulingana na hadhi yake, lakini hamkumbuki dereva kuwa uwezo wake wa kununua chakula kwenye hoteli hiyo ni mdogo, jambo ambalo linaathiri maisha yake.

Wakati dereva anafanyiwa haya yote ndiye anamwendesha kiongozi mkubwa wa taasisi kubwa ambayo inamtegemea kiasi kwamba ikitokea amefariki kwa sababu ya ajali ni pigo kwa kampuni au familia.

Baadhi huwaendesha mabosi hadi usiku wa maanani na wanatakiwa kuacha gari eneo maalum, ndipo waende nyumbani na mara nyingi hutegemea anakoishi na aina ya bosi kama ana huruma na atamsaidia nauli ya usafiri usiku huo, na wakati huo anatakiwa kuwahi alfajiri kumchukua bosi kumuwahisha kazini.


Ni muhimu msisitizo wa mikataba na maslahi bora ya madereva kazini ikasimamiwa ipasavyo, ili kuhakikisha wanakuwa na hali bora kazini kutokana na umuhimu wao kwa mabosi na nchi kwa ujumla.

Kama ambavyo kampuni, mashirika au serikali inajipanga kuajiri wataalamu mbalimbali ni muhimu kutazama madereva wa sekta zote ikiwamo wa magari ya abiria.

Hivyo, pamoja na kutaka kuharakisha ajira za madereva, lakini ni muhimu kujali hali za madereva ikiwamo muda wa kuingia na kutoka kazini, stahiki nje ya mshahara, muda wa kuwasubiri mabosi, na kupata chakula na vinjwaji wanapokuwa kwenye mikutano, kwa kuwa baadhi ya mikutano madereva husahaulika na kuishia kula makombo.

Madereva huficha siri nyingi za familia, kampuni, mashirika na serikali kwa kuwa muda mwingi wako na bosi ni rahisi kusikiliza maongezi yake na kuona mienendo yake, na ni rahisi kumdhuru na kwa umuhimu huo lazima kumjali, lakini zaidi kama binadamu mwenzako.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wazalishaji vifungashio plastiki msisahau marufuku wiki 4 zijazo

Na Sabato Kasika

**KUANZIA** mwezi ujao, yaani Aprili 8, mwaka huu, utakuwa mwisho wa kutumia vifungashio vya plastiki kubebea bidhaa. Baada ya hapo itakuwa ni marufuku mtu kuzalisha, kuuza, kusambaza na kuvitumia.

Kufikia tarehe hiyo, kwa lugha rahisi ni wiki nne zijazo, itakuwa imetumia miezi mitatu ya rehema iliyotolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ummy Mwalimu, kuhakikisha vifungashio hivyo havipo tena sokoni.

Waziri Ummy anasema, baada ya hapo itakuwa ni kinyume cha sheria kutumia kwa namna yoyote vifungashio na kwamba atakayekutwa navyo, atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Hatua ya serikali kufikia uamuzi huo, inatokana na kuwapo vifungashio vinavyotumika kama vibebeo vilivyozagaa madukani, sokoni na maeneo mbalimbali, vinavyoshindwa kukidhi mtakwa ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Anasema vifungashio hivyo vinazalishwa kwa wingi na kwa ukubwa tofauti, na vinatumika kama mifuko ya kubebea bidhaa sokoni, hata kuleta dhana kuwa mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku imerudi kivingine.

Kufanikisha marufuku ya kuwapo kwa vifingashio hivyo, wasambazaji, wazalishaji na waagizaji wanatakiwa kuacha mara moja kuzalisha, kusambaza, kuuza na kutumia vifungashio hivyo.

Hivyo, ni wazi kuna haja wahusika wakazingatia maelekezo hayo kwa kuwa baada ya Aprili 8, serikali inasema haitatoa tangazo lingine lolote kuhusiana na katazo la matumizi ya vifungashio visivyokuwa na ubora.

Uzoefu unaonyesha kuwapo wajanja wachache wanaopenda kuongezewa muda, wakidai kwamba wana bidhaa nyingi walizozalisha kabla ya tangazo, hali inayokwamisha lengo lililokusudiwa.

Hali kama hiyo imewahi kujitokeza hata pale TBS ilipopiga marufuku kuhusu uingizwaji nguo za mitumba, zikiwamo za ndani. Wafanyabiashara waliongezewa muda kama walivyoomba.

Kinyume chake ni kwamba, biashara hizo ziliendelea kama kawaida, kwa kuwa wapo baadhi waliokuwa wakiagiza nguo hizo na kuziingiza nchini kwa njia za 'panya' hali inayokwamisha marufuku ya TBS, ambayo kwa njia pana, ni mdomo wa serikali.

Mtindo huo wa kuomba kuongezewa muda uko kwa wengi, wakiwamo wahusika wa mifuko ya plastiki. Nao tuliwashuhudia wakiongezewa muda na ukomo huo ukoo huo ulipofika, haukuongezwa mwingine. Matokeo yake, hadi sasa hakuna mifuko ya plastiki madukani wala mitaani, kwa kuwa inawezekana kama serikali ingeendelea kuongeza muda, wafanyabiashara nao wangeendelea kuzalisha mifuko mingine zaidi. Sasa kwenye vifungashio vya plastiki, serikali inasema itachukua hatua kali za kisheria na inaendelea na operesheni maalumu kuwabaini watakaokwamisha mafanikio hayo kwa kuzalisha na kusambaza vifungashio hivyo.

Kinachotakiwa sasa ni watumiaji vifungashio, wasambazaji, wauzaji na wazalishaji kujipanga kwa ajili ya mabadiliko yanayokuja, ili iwe kama ilivyokuwa baada ya marufuku ya mifuko ya plastiki.

Wafanyabiashara wadogo wakiwamo wa ubuyu, karanga, vipande wa vya miwa, nyanya, karoti na vingine ni wateja wakubwa wa vifungashio hivyo. Ni vyema sasa wakajipanga kwa ajili ya mabadiliko yajayo.

Binafsi ninaamini kwamba, serikali iliweka miezi mitatu kwa kuzingatia hali halisi ya wafanyabiashara wadogo ambao ni watumiaji wa mwisho, ili wajipange kwa ajili kununua vifungashio vyenye ubora zaidi.

Serikali inabainisha kuwa, TBS ina kanzidata ya wazalishaji wa kutosha wa vifungashio vyenye viwango, na inaweka wazi kuwa hakutakuwa na uhaba wa vifungashio vinavyokidhi viwango, baada ya Aprili 8 mwaka huu.

Kwa maelezo hayo ya waziri, ni vyema wazalishaji na wawekezaji wa ndani kuchangamkia fursa hiyo kwa kuzalisha vifungashio vinavyokidhi viwango ili kujihakikishia soko la bidhaa hizo.

Yaliyotokea miaka ya nyuma ya baadhi ya wafanyabiashara na wazalishaji kudai wana 'mzigo mkubwa' waongezewe muda waumalize na kumbe lengo ni kutaka kuendelea kuingiza au kuzalisha si sahihi hata kidogo kwa maslahi ya taifa.

Jambo la msingi ni kwa wahusika kuzingatia maelekezo ya serikali, ikiwamo ya mifuko kuwa na nembo ya TBS kuonyesha kuwa imekidhi vigezo vinavyotakiwa, pamoja na kutambulisha jina la mzalishaji.

Vilevile kuna kigezo kingine kinachotajwa ambacho ni lakiri (seal), inayomaanisha kuwa imefungashwa na mzalishaji kabla ya kwenda sokoni.

# Madai biashara ya heroin yawafikisha mahakamani

**Na Hellen Mwango**

WAKAZI wanne wa Kinondoni jijini Dar es Salaam, akiwamo mfanyabiashara, Said Mbasha (24), wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka ya kufanyabiashara ya dawa za kulevya aina ya heroin na kukutwa na kilo 30.6.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Joseph Dalidali (27), Allu Murungwa (24) na Fatuma Shomari (24).

Walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi Godfrey Isaya katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali, Wankyo Simon, alidai Machi 3, mwaka huu, eneo la Kijitonyama, Mkoa wa Dar es Salaam, washtakiwa wote walijihusisha na biashara ya dawa za kulevya kilo 30.6 za heroin.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Machi 3, mwaka huu, katika mtaa wa Kasaba, Kinondoni Dar es Salaam, Mbasha na Fatuma walikutwa na dawa za kulevya aina ya bangi gramu 2.63.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na uliomba mahakama kupanga tarehe ya kutajwa.

Hakimu Isaya alisema kesi hiyo itatajwa Machi 24, mwaka huu na washtakiwa wapelekwe mahabusu kwa sababu mashtaka ya kesi hiyo hayana dhamana.

**Wakili wa Serikali, Wankyo Simon, alidai Machi 3, mwaka huu, eneo la Kijitonyama, Mkoa wa Dar es Salaam, washtakiwa wote walijihusisha na biashara ya dawa za kulevya kilo 30.6 za heroin.**



Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya MECCO, wakiweka mifereji ya maji eneo la Kontena Mivumoni, katika ujenzi unaoendelea wa barabara ya Wazo hadi Madale kwa kiwango cha lami, Manispaa ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Majaliwa atoa siku 3 malipo ya wakulima

**Na Mwandishi Wetu,**
NJOMBE

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameipa siku tatu kuanzia juzi kampuni ya DL iwasilishe maelezo ya kwanini hajawalipa wakulima wa chai fedha zao tangu mwaka jana na kusababisha washindwe kuhudumia mashamba yao.

Alitoa agizo hilo juzi alipohitimisha kikao na wadau wa zao la chai kilichofanyika katika Ukumbi wa Johnson mjini Njombe.

Ilibainishwa katika kikao hicho kwamba uzalishaji wa chai kavu umeshuka kutoka tani 37,192 kwa mwaka 2018/19 hadi tani 28,715 kwa mwaka 2019/20 kutokana na sababu mbalimbali.

Waziri Mkuu aliitaka Bodi ya Chai Tanzania ihakikishe inasimamia ipasavyo zao hilo ili wakulima wanufaike, akiagiza:

"Bodi wajibikeni kwa kusimamia ipasavyo bei ya chai na wawezesheni wakulima waelewe mfumo unaotumika katika kuuza zao hilo."

Majaliwa alitoa agizo hilo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wawakilishi wa wakulima ambao walidai kuwapo tofauti katika bei ya chai. "Suala la bei lizingatiwe, mifumo inayotumika katika kuuza chai ieleweke kwa wakulima," Majaliwa aliagiza.

Akizungumzia upatikanaji wa pembejeo, Majaliwa alisema serikali itahakikisha zinapatikana ili kumwezesha mkulima kufanya kazi yake kwa urahisi na ufanisi zaidi.

Waziri Mkuu aliiagiza Wizara ya Kilimo ihakikishe inatengeneza utaratibu wa kukutana na wadau ili kujua kero na matatizo yanayowakabili na kushirikiana nao katika kuyatafutia ufumbuzi.

Aliitaka wizara hiyo isimamie uanzishwaji wa vyama vikuu vya ushirika wa wakulima wa chai katika maeneo yanayolima zao hilo na vihakikishe vinakuwa na viongozi wenye nia ya dhati ya kuuendeleza ushirika huo na kuongeza tija kwa wakulima.

Waziri Mkuu pia aliiagiza Bodi ya Chai Tanzania (TBT) na Taasisi ya Utafiti wa Chai (TRIT), wahakikishe wanawafikishia wakulima miche bora na viuatilifu vinavyotakiwa kwa wakati ili waongeze ubora wa chai inayolimwa nchini.

Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda, alisema wizara itayafanyia kazi maagizo yote yaliyotolewa na Waziri Mkuu pamoja na maoni ya wadau ili kuhakikisha zao hilo linaboreshwa.

Kuhusu kero ya miundombinu ya barabara ziendazo katika mashamba ya chai, waziri huyo aliahidi kuzungumza na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), ili kuhakikisha zinapewa kipaumbele.

# 'Mashetani' yadaiwa kushika mwanafunzi

**Na Shufaa Lyimo**

MWANAFUNZI wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Tabata jijini Dar es Salaam (jina tunalihifadhi), hajaripoti shuleni tangu kufunguliwa kwa mwaka huu wa masomo kutokana na kile kinachodaiwa anasumbuliwa na 'mashetani'.Kwa mujibu wa mama mwanafunzi huyo ambaye aliomba hifadhi ya jina lake, mwanafunzi huyo hajaripoti shuleni mwaka huu kutokana na tatizo hilo.

Alidai kuwa mwanawe huyo mara nyingi anapokuwa anakwenda shuleni, huanguka na kupoteza fahamu kwa muda mrefu, hivyo wamelazimika kumfungia ndani.

"Ni kweli tangu mwaka jana mwanangu hajaenda shuleni kwa sababu mara nyingi akiwa anajiandaa kwenda shule, anapatwa na usingizi ambao utamchukua saa nyingi. Hadi kuamka, muda wa shule unakuwa umeshapita, analazimika kubakia nyumbani," alidai.Mama huyo alidai kuwa mbali na kupatwa na usingizi mzito, kuna wakati mwanawe huyo alikuwa anakwenda shule, anapokaribia maeneo ya shule, anaanguka na kupoteza fahamu kwa takribani saa nzima.

Mzazi huyo alidai kuwa kwa sasa ameyumba kiuchumi kutokana na kutumia fedha nyingi kutafuta ufumbuzi wa tatizo linalomkabili mwanawe.

Alisema wamelazimika kumfungia ndani mwanafunzi huyo kwa kuwa wakimruhusu kutoka, anakwenda kutembea kusikojulikana na kurejea nyumbani saa tisa usiku.

"Huyu ni mtoto wa pekee wa kike katika familia. Ninao wengine wawili wa kiume. Ninaumia kuona mwanangu anashindwa kuendelea na masomo, nilikuwa nimepanga kumfanyia mambo makubwa kielimu kwa sababu ninatambua umuhimu wa elimu hasa kwa mtoto wa kike," alisema.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Alex Mugisha, alisema mpaka sasa hajapata taarifa rasmi kuhusu sababu za utoro wa mwanafunzi huyo zaidi ya wanafunzi wenzake kubainisha kwamba wanamuona mitaani.

"Endapo tutabaini mwanafunzi huyo kweli amefungiwa bila ya kuwa na tatizo lolote, tutawachukulia hatua kali wazazi wake kwa sababu tunataka tufuate agizo la Rais wetu, Dk. John Magufuli, katika sekta ya elimu," alisema mwalimu huyo.

Alibainisha kuwa kwa sasa shule yake imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kupunguza utoro miongoni mwa wanafunzi, tofauti na mwaka uliopita ambao utoro ulikuwa umekithiri.

Mwalimu huyo alibainisha kuwa kutokana na kadhia hiyo, watahiniwa 17 kutoka shule yake, walifeli Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba mwaka jana, kati ya 227 walioufanya.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Msimbazi Magharibi, Hamza Ramadhani, aliiambia Nipashe jana kuwa alikuwa hajatapa taarifa za utoro wa mwanafunzi huyo huku akiahidi kulifanyia kazi suala hilo.

## Wilaya Magu yatakiwa mipango sahihi ya ardhi

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Magu mkoani Mwanza (Idara ya Ardhi), imetakiwa kuweka mipango sahihi ya ardhi ili kuondoa ujenzi holela na migogoro katika maeneo mbalimbali ya wilayani humo.

Hayo yalibainishwa na Diwani wa Bujashi wilayani Magu, Deleli Mazoya, wakati akikabidhi hati ya kiwanja, kibali cha ujenzi pamoja na ramani kwa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mwanza (MPC).

Kiwanja hicho kipo eneo la mradi wa Isangijo Satellite City uliopo kwenye wilayani Magu.

Deleli alisema Idara ya Ardhi inatakiwa kutatua migogoro iliyopo kati ya wawekezaji wanaojenga viwanda na wananchi wenye makazi kwa kuchora michoro inayoonyesha maeneo ya makazi ya watu na viwanda.

"Nitoe wito kwa watu wa ardhi waweke mipango sahihi, ukiangalia majengo yanajengwa kiholela, tunazidiwa na babu zetu ambao wakati wa operesheni vijiji waliweza kupanga vizuri kabisa miji, na ukiangalia unajua kabisa hapa kuna barabara, lakini sasa watu wanajenga kiholela tu, mfano ukiangalia hapo Kisesa hapakaliki mji umejaa ovyo," alisema Deleli.

Diwani huyo aliwaomba waandishi wa habari kutumia taaluma yao kuwaelimisha watu badala kuwapotosha kwa ajili ya kutunza amani na kuleta maendeleo ya nchi.

Mwenyekiti wa MPC, Edwin Soko, alisema, klabu hiyo ilichukua kiwanja katika eneo hilo ili kusogeza huduma za habari karibu na wananchi.

Aidha, alisema MPC itahakikisha waandishi habari wanawake wanapata viwanja kwenye mradi huo kwa kuamini kuwa wana haki ya kumiliki ardhi kama ilivyo kwa wengine.

## Wenyeviti watakiwa ushirikishaji wananchi

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

WENYEVITI wa Serikali za Vijiji mkoani Tabora wametakiwa kujenga utamaduni wa kuwashirikisha wananchi katika upangaji na utekelezaji wa shughuli na miradi ya maendeleo katika maeneo yao ili iwe endelevu.

Maelekezo hayo yalitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo Wenyeviti wa Vijiji, Watendaji, Wakuu wa Idara na Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo.

Alisema hatua itajenga imani kubwa kwa wananchi na kuwa walinzi wa miradi itakayoibuliwa katika maeneo yao kwa sababu wamechangia katika uanzishwaji wake.

Sengati alisema ushirikiano kati ya viongozi wa vijiji na wananchi utasaidia kuimarisha amani na kuchochea maendeleo katika vijiji vyao.

Mbunge wa Urambo, Margeret Sitta, alisema lengo la mafunzo hayo kwa wenyeviti wa vijiji, watendaji wa kata na madiwani ni kuwajengea uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa usahihi katika kuwaletea maendeleo wakazi wa wilaya hiyo.

Alisema kuwa yanalenga kuwaongezea uwezo wa kuandika maandiko ya kuibua miradi ya maendeleo katika maeneo yao kwa ajili ya kuwasaidia wanakijiji wanaowaongoza.

# Wizara kuboresha ufugaji samaki

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema serikali imeweka lengo la kuhakikisha sekta ya uvuvi kupitia ufugaji samaki inazalisha idadi kubwa ya samaki hasa wanaopatikana kwenye vyanzo vya maji vya asili.

Akizungumza jana alipokagua shughuli zinazofanywa na Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji cha Kingolwira mkoani Morogoro, Waziri Ndaki alisema sekta ya ufugaji samaki imekuwa na mwitikio mkubwa kwa sasa kutokana na mahitaji ya soko lake kuongezeka.

Alisema wizara hiyo itahakikisha inaendelea kuboresha miundombinu ya uzalishaji vifaranga vya samaki na kupanua zaidi wigo wa uzalishaji wake ili viende sambamba na mahitaji ya vifaranga kwa watu wanaofuga samaki.

Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji wa Wizara hiyo, Dk. Nazael Madalla, alisema wapo katika hatua mbalimbali za kuendelea kutoa elimu kuhusu ufugaji wa samaki ikiwamo kwa kutumia simu za mkononi.

Alisema kupitia uboreshaji unaofanyika katika Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji cha Kingolwira, wapo mbioni kuanza uzalishaji wa vifaranga vya samaki aina Kambale.

Pia alisema vituo vya ukuzaji viumbe maji vilivyo chini ya Wizara ya hiyo Uvuvi vimeanza kuuza vifaranga aina ya sangara.

Kaimu Ofisa Mfawidhi wa Kituo hicho, Hamady Makorwa, alisema mkakati wao ni kuendeleza shughuli za uzalishaji ili kufikia lengo la kuzalisha vifaranga 600,000 kwa mwezi.

Alisema ili kufikia lengo hilo, kituo kinahitaji mabwawa 26 na Samaki aina ya Sato kwa ajili ya kuzalisha vifaranga 24,000 ambao kwa sasa wapo 5,430.



Mmachinga akihamisha mbao za banda lake, baada ya vibanda vya wafanyabiashara vilivyokuwa pembeni mwa ukuta wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO) Ubungo, jijini Dar es Salaam kubomolewa mapema wiki hii. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Watendaji waagizwa kusimamia miradi ya maji

**Na Said Hamdani,** LINDI

SERIKALI mkoani Lindi, imewaagiza wakurugenzi watendaji wa halmashauri, manispaa na miji midogo, kuwaelekeza watendaji wa kata kusimamia miradi ya maji na vyanzo vyake katika maeneo yao ili kila mtu aweze kunufaika na upatikanaji wa huduma hiyo muhimu.

Agizo hilo limetolewa na Kaimu Mkuu wa mkoa huo, Shaibu Ndemanga, wakati wa kufunga kikao cha wadau wa sekta ya maji, mkoa kilichofanyika mjini hapa. Alisema serikali imedhamiria kupambana kuhakikisha wananchi wanaondokana na kadhia ya upatikanaji wa huduma hiyo, huku akiwataka watumishi wa wakala wa maji na usafi wa mazingira mijini na vijijini (LUWASA na RUWASA), kutekeleze majukumu yao bila hofu.

Alisema serikali inapambana kuhakikisha fedha zinapatikana na kuletwa Mkoa wa Lindi kwa wakati ili utekelezaji wa kuwapatia wananchi, wakiwamo kinamama huduma bora.

Akitoa taarifa ya utekelezaji, Meneja Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira (RUWASA), Mkoa wa Lindi, Muhibu Lubasa, alisema viwango vya upatikanaji wa maji yameongezeka kutoka asilimia 58 mwaka 2019 hadi 64 kufikia Desemba, mwaka huu.

Alisema wakati RUWASA imeanza kazi Juni 2019, upatikanaji wa maji ulikuwa asilimia 58 na hadi Desemba 2020, kiwango kimeongezeka na kufikia asilimia 64, huku vijiji 268 vilivyo na huduma chini ya asilimia 40 vimeainishwa na kupewa kipaumbele.

Alisema kipindi cha mwaka mmoja na nusu, wametekeleza zaidi ya miradi 50 inayohudumia wananchi wapya 80 na kuongeza upatikanaji wa huduma hiyo, huku akitaja sababu za ongezeko hilo, serikali kuwekeza katika sekta ya maji mkoani humo, maeneo ya vijijini.

Alisema RUWASA imekamilisha usanifu wa miradi mitatu ya kimkakati, kwa Wilaya ya Lindi, Navanga Corridor katika vijiji vinane, Rondo sita na Mbwinji, huku wilaya za Nachingwea na Ruangwa, jumla ya vijiji vilivyoainishwa ni 54 kati ya hivyo 34 vipo Wilaya ya Ruangwa.

# Wafugaji nguruwe wataka kukatiwa bima

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAFUGAJI wa nguruwe, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama Mjini, wameiomba serikali kuwaingiza kwenye mfumo wa bima za wanyama kama ilivyo kwenye vyombo vya moto, ili kuepuka na hasara ambayo wamekuwa wakiipata unapoingia ugonjwa wa homa ya nguruwe.

Mwisho mwa mwaka jana, uliingia ugonjwa huo, Wilaya ya Kahama na kusababisha nguruwe zaidi ya 500 katika mazizi matano ya wafugaji kufa na mwanzoni mwa mwaka huu, serikali ilisitisha biashara ya usafirishaji na uuzwaji wa nyama ya nguruwe mpaka tiba ilipopatikana.

Benny Mao, mwenyekiti wa kikundi cha Tujipambanue kaya ya Mwendakulima, aliyabainisha hayo juzi walipotembelewa na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), Patrobas Katambi, alisema, mwaka 2017 uliingia ugonjwa wa homa kali ya nguruwe kwa mara ya kwanza na kusababisha nguruwe wengi kufa.

Mao ambaye ni mwenyekiti wa wafugaji, alisema kama serikali ingewapatia bima za wanyama hao, wasingeendelea kupata hasara ya mifugo wanayopata, kwani wanawekeza fedha nyingi zinazopatikana na mikopo inayotolewa na halmashauri, lakini wanashindwa kuilipa kwa wakati hasa wakati wa ugonjwa huo.

"Kikundi chetu kina nguruwe 338 na asilimia kubwa ya fedha za uanzishaji wa mradihuuzinatokananamikopo inayotolewa na halmashauri yetu, mwanzo walitupatia shilingi milioni nane ambazo mpaka sasa tumesharejesha na tumeomba mkopo mwingine wa shilingi milioni 10," alisema Mao.

Aidha, alisema, gharama za uendeshaji wa mradi huo ni kubwa na kwa mwezi wanatakiwa kuwahudumia kwa chakula na madawa wanyama hao kwa kiasi cha Sh. milioni sita, lakini wanawahudumia Sh. milioni 3.8 matumizi ambayo hayakidhi mahitaji.

Naibu Waziri Katambi alisema bima hizo zipo na zinatolewa na serikali na taasisi binafsi ikiwamo taasisi za kifedha na zinasaidia kutoingia kwenye hasara linapotokea tatizo hasa unapoingia ugonjwa wa homa kali ya nguruwe.

Alisema bima ya mifugo inaweza kuwa inatolewa kwa gharama ndogo sana ukilinganisha na bima za magari na nyumba na kuwataka kuhakikisha kila mfugaji anakata bima za wanyama wake ili kuondokana na hasara ya kufa kwa mifugo.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya, alisema ugonjwa wa homa ya nguruwe uliingia na serikali ikaamua kusitisha biashara ya nyama na usafirishaji wa nyama hiyo, lakini kwa sasa biashara imefunguliwa, ila bado tunaendelea kuzuia katika Kata ya Kagonjwa.

# TADB yatakiwa kuwekeza utafiti mbegu bora

**Na aMwandishi Wetu,** KATAVI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (Uwekezaji), Prof. Kitila Mkumbo, ameishauri Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kushirikiana

na taasisi za utafiti katika kuzalisha mbegu bora ili sekta ya kilimo iimarike, itoe malighafi za viwanda na kuimarisha zaidi usalama wa chakula wa taifa.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya uzinduzi wa kitabu cha mwongozo wa uwekezaji wa Mkoa wa Katavi, Prof. Mkumbo alisema ni

vizuri TADB kuongeza juhudi katika kufanya mageuzi makubwa katika kilimo kwa kushirikiana haraka na taasisi za utafiti kuzalisha mbegu bora ili taifa limkakati liimarishe zaidi usalama wa chakula, lipate malighafi za viwanda kwa urahisi na kwa uhakika na ziada ya mazao

iuzwe nchi za nje.

Amesema ili shabaha hiyo ifikiwe, lazima pawepo na mikakati madhubuti ya kuunganisha juhudi za taasisi za kitaifa na ziwe na lengo moja hasa katika kipindi hiki ambacho taifa linatekeleza azma ya

ujenzi wa uchumi wa viwanda.

"Azma ya serikali ni kujenga uchumi wa viwanda ifikapo 2025. Hatuwezi kuongelea viwanda kama sekta ya kilimo, ambayo ni mzalishaji mkubwa wamalighafi za viwanda, haitafanyiwa mageuzi makubwa. Jambo ambalo wanaweza kufanya TADB ni kuanza kuwezesha taasisi za utafiti za kilimo

ikiwamo Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) na zingine ili kuwa na mbegu bora ambazo zitaongeza uzalishaji katika kilimo na hivyo kuwa na malighafi za kutosha kwa viwanda vya ndani," amesema Prof. Mkumbo.

Waziri Mkumbo alipongeza jitihada za TADB za kuhakikisha nchi inakuwa na usalama wa chakula, na kwamba benki hiyo imesaidia sana juhudi za

taifa ya kuongeza thamani ya mazao na kwa upande wa Mkoa wa Katavi benki hiyo imesaidia zaidi ya viwanda 30 vya kuchakata mazao mkoani

humo.



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakiendelea na matengenezo ya bomba chakavu eneo la Kawe, mkoani humo jana. Mamlaka hiyo, inaendelea kubadilisha mabomba chakavu ili kupunguza kiwango cha maji yanayopotea. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafungwa wanawake wawezeshwa runinga

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

UMOJA wa wanawake waishio mjini Masasi, wametoa msaada wa Tv na king'amuzi cha Azam Tv kwa wafungwa wanawake wanaotumikia vifungo vya mbalimbali katika Gereza la Wilaya ya Masasi.

Msaada huo waliutoa ikiwa ni mwendelezo wa msaada wa vifaa mbalimbali walivyotoa katika gereza hilo kwa wafungwa wanawake katika wiki ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambapo kilele chake kilikuwa Jumatatu.

Kiongozi wa umoja huo, Zuwena Ungele, alisema wametoa msaada huo kutokana na kuguswa na mahitaji wanayohitaji wakiwa kama wafungwa ikiwamo kupata taarifa mbalimbali za habari zinaendelea kutokea nchini na duniani.

Ungele alisema kwa kupata msaada huo, sasa wafungwa hao watapata fursa ya kufahamu taarifa za habari wakiwa gerezani tofauti na awali ambapo walikuwa wapweke.

Mkuu wa gereza hilo, Ayubu Mwenda, aliwashukuru wanawake hao kwa kufika hapo na kutoa msaada huo kwa wafungwa wanawake.

# Benki UBA yaja na usawa kijinsia

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya UBA, imesema itahakikisha inaendelea kuimarisha mkakati wa kuzingatia usawa wa kijinsia kazini na katika maisha ya kawaida kwa wafanyakazi wake.

Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano, Brendansia Kileo, alisema katika kufanikisha kuweka usawa wa kijinsia katika maisha ya kazi na maisha ya kawaida, kuna umuhimu pia wa makundi yote ya wanaume na wanawake kushirikiana ili kuleta maendeleo chanya.

"Na ndio maana katika kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani ambayo ilifanyika Machi 8, mwaka huu, sisi wanawake wa UBA tumewajumuisha wanaume ili kupata mawazo yao wanayoyafikiria katika kushirikiana na kuwaunga mkono katika kutimiza ndoto zetu kwenye majukumu ya kila siku, tunapokuwa kazini na nyumbani," alisema Kileo.

"Na wanawake wengi kwenye jamii wanashindwa kutimiza ndoto zao kwa wakati mwingine kwa kuzidiwa na majukumu ya kazi na ndiyo maana UBA tumeandaa mikakati mbalimbali ambayo itawasaidia kufikia malengo yao."

Alisema wanawake na wanaume kushirikiana katika shughuli mbalimbali kutasaidia kufikia malengo kwa haraka zaidi iwe katika maisha ya kawaida au kazini.

# Ujenzi wa reli ya kisasa Mwanza - Isaka waanza

**Na Anthony Ishengoma**

SERIKALI imeanza ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha Isaka-Mwanza wenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni moja.

Mradi huo unatarajiwa kuzinufaisha pia nchi jirani za Uganda, Rwanda na Burundi pamoja na mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Mkurugenzi wa Shirika la Reli, Masanja Kadogosa, akizungumzia kuanza kwa mradi huo jana, alitaja faida za mradi huo kwa wakazi wa Kanda ya Ziwa kuwa utarahisisha usafiri kwenda Dodoma na Dar es Salaam pamoja na Bandari Kavu ya Isaka itakayotumika kupokea na kushusha mizigo yote ya nchi jirani.

Kadogosa alisema ujenzi wa reli hiyo utaenda sambamba na upanuzi wa Bandari Kavu ya Isaka kwa lengo la kuiongezea ufanisi.

Alisema ujenzi wa reli hiyo ni fursa kubwa kwa wakazi wa Shinyanga kwa kuwa watapata ajira na ujuzi kwa kushiriki katika mradi huo mkubwa utakaoachukua miezi 36 mpaka kukamilika kwake.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, akizungumza katika Bandari Kavu ya Isaka, aliwaka watekelezaji wa mradi huo kuzingatia umuhimu wa kuwa na kipande kidogo cha reli kuelekea eneo la viwanda lililoko Manispaa ya Kahama.

Telack alihaidi kutoa ushirikiano katika nyanja zote zinazotakiwa kufanyiwa kazi ikiwamo kuwaandaa wananchi kupokea mradi huo.

Diwani wa Isaka, Pazi Majuto, aliongeza kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo, akiwataka wananchi kuchangamkia fursa za ajira na biashara katika mradi huo.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, akifafanua jambo kwa Mkurugenzi wa Shirika la Reli nchini, Masanja Kadosa (kushoto), eneo la viwanda Manispaa ya Shinyanga, kuangalia reli ya kisasa itakavyosaidia usafirishaji wa mazao na bidhaa za viwanda. Wapili kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Yasinta Mboneko. **PICHA: ANTHONY ISHENGOMA**

# Aona fursa kiwanda usafishaji dhahabu

**Na Asteria Muhozya,**
DODOMA

KUKAMILIKA kwa ujenzi wa kiwanda cha kusafisha dhahabu cha Mwanza Precious Metals Refinery Ltd, kunatarajiwa kuleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi mkoani huko na taifa kwa ujumla.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Dk. Venance Mwasse, alibainisha hayo juzi alipotoa taarifa kuhusu utekelezaji wa mradi huo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini jijini Dodoma.

Kiwanda hicho kinachotajwa kuwa na teknolojia ya kisasa ya kusafisha dhahabu kinatarajiwa kuiongezea ubora dhahabu kutoka Tanzania, hivyo kununuliwa na Benki ya Dunia kwa ajili ya kuhifadhiwa.

Dk. Mwasse alisema kiwanda hicho kitaongeza uzalishaji hadi kilo 960 kwa siku ikiwa ni sawa na mara mbili ya uzalishaji wa sasa.

Alisema ujenzi wa kiwanda hicho ambacho ni kikubwa kwa usafishaji dhahabu kulinganishwa na mitambo ya nchi za Afrika ya Kusini na Sudan, ni matokeo ya marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2017, ambayo yaliweka msisitizo kuhusiana na rasilimali za nchi na matakwa ya nchi kufaidika na madini yanayochimbwa nchini kwa kuyaongezea thamani kabla ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi.

Akizugumzia vyanzo vya malighafi katika kiwanda hicho, mkurugenzi huyo alisema zitatoka kwa wachimbaji wadogo kupitia mradi wa kusaidia wachimbaji wadogo, wachimbaji wakubwa wenye migodi nchini, dhahabu kutoka nchi jirani na dhahabu kutoka kwa madalali.

Alisema ujenzi wa kiwanda hicho utaongeza mapato kwa nchi kupitia mrabaha na ada za ukaguzi, kuongeza mapato ya halmashauri kiliko kiwanda hicho kupitia ushuru wa huduma na kuongeza ajira kwa taifa ambapo mradi unatarajia kuajiri watu 120, wengi wakiwa Watanzania.

Faida zingine alizitaja kuwa ni kuwezesha Benki Kuu kuanza kununua dhahabu kwa mujibu wa sheria za nchi, serikali kuanza kukusanya mrabaha kwa kuchukua dhahabu badala ya fedha, dhahabu inayozalishwa Tanzania kuanza kutambulika na kuwa na nembo yake maluum, kuwa na kituo cha kuuza dhdhabu kutoka kwa wazalishaji wa ndani na nje ya nchi na huduma kwa jamii inayozunguka mradi huo.

Mradi wa Mwanza Precious Metals Refinery ni ubia kati ya STAMICO, Kampuni ya Rozelia General Trading LLC ya Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Kampuni ya ACME Consultant Engineers PTE Ltd ya Singapore. STAMICO inamiliki asilimia 25.

# Watanzania wanaozungumza Kifaransa wafikia milioni 1.5

**Na Salome Kitomari**

IDADI ya Watanzania wanaozungumza Kifaransa, imefikia milioni 1.5, ikiwa ni lugha pekee ya kigeni baada ya Kiingereza kinachotumika kwenye mitaala ya kufundishia.

Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, alibainisha hayo juzi katika mkutano na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Lugha ya Kifaransa, uliofanywa na mabalozi wa nchi za Ufaransa, Ubelgiji, Canada, Morocco, Uswisi na Comoro.

Alisema kwa kushirikiana na serikali, wamekuja na programu ya kufundisha walimu ambao watakwenda kufundisha Kifaransa shuleni na kila mwaka watawafikia kati ya 50 hadi 100 huku lengo likiwa ni kufikia 1,000 baada ya miaka 10.

"Kwenye nchi za Ulaya, Kifaransa ni lugha ya pili inayotumika zaidi sekondari, ukiziondoa nchi ambazo Kifarasansa ni lugha mama. Mkoani Kigoma wazungumzaji wa Kifaransa ni asilimia sita huku wastani wa nchi kuwa ni asilimia mbili," alisema.

Balozi Clavier alisema kuna wazungumzaji milioni 300 wa Kifaransa na inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2070, idadi itafikia milioni 800 huku wengi wao wakiwa ni wa Afrika.

Alisema Kifaransa ni lugha rasmi katika mataifa 32 duniani na inatumika katika vikao vya wakuu wa nchi za Afrika Mashariki na ni lugha inayosomwa na watu zaidi ya milioni 32 katika nchi 36 na ya nne inayotumika kwenye intaneti.

Kwa mujibu wa balozi huyo, Kifaransa ni lugha ya kimataifa ya pili inayotumika kwenye vyombo vya habari na ya tatu kwenye biashara na ikisalia kuwa ya pili kutumika katika taasisi za kidiplomasia duniani.

Alisema asilimia 59 ya wazungumzaji wa Kifaransa wanaishi Afrika, huku idadi hiyo ikitarajiwa kuongezeka kufikia asilimia 80 mwaka 2050, huku kukiwa na nchi 21 zinazotumia lugha hiyo kama lugha rasmi.

Balozi wa Ubeligiji nchini, Peter Van Acker, nchini kwao watu huzungumza lugha mbalimbali zikiwamo Kiholanzi na Kijerumani huku nusu ya wananchi wakizungumza Kifaransa.

Balozi wa Canada nchini, Pamela O'Donnel, alisema katika maadhimisho hayo ya wiki mbili, kutakuwa na maonyesha ya kazi za sanaa za muziki na michoro pamoja na vipindi maalum vya masuala ya mazingira.


Ukurasa 12

Kutana na mwanamama dereva wa malori kuvuka mipaka nchi jirani



Ukurasa 13

Mheshimiwa Rais kero si maji tu, pia umeme


# BUFE

IJUMAA MACHI 12, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

## Bosi TPDC achambua uchumi gesi unavyokaribisha Tanzania Viwanda

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

# Kiwanda rasmi cha kinamama wa Sengerema, kila kitu ni wao

• Mazao kuharibika 'stop', mifugo faida tupu

**Na Clara Matimo**

AHADI mojawapo ya kiserikali ambayo inatekelezwa hadi sasa, ni kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara na wajasiriamali, yatakayowasaidia kuendesha viwanda, ikiaminika ndio mwarobaini wa kuliinua taifa kiuchumi.

Ni hali inayofungua milango ya ajira na misukumo mingine ya maendeleo, kulingana na mitaji, ujuzi na ngazi za tofauti kielimu.

Tayari kuna asasi mpya na za kale, kutoka ndani na nje ya nchi zinahamasika kushiriki maendeleo ya taifa, ikiwamo Shirika lisilo la Serikali Mikono Yetu, jijini Mwanza, lililojikita kuwawezesha kinamama kumiliki rasilimali zalishi, kama ardhi na mifugo wajikwamue.

Mikono Yetu inajenga kiwanda mahsusi cha wanawake katika Kata ya Kahumulo, wilayani Sengerema, mkoani Mwanza, pamoja na kuwatengea eneo la soko.


Kinamama wakibeba tofali za ujenzi wa kiwanda chao, huko Sengerema mkoani Mwanza. **PICHA: CLAR A MATIMO**

Meneja Programu wa Mikono Yetu, Sophia Nshushi, anasema ni kiwanda kitakachochakata bidhaa za mifugo na mazao kilimo, kwa matarajio ya kunufaisha wanawake zaidi ya 150, ikigharimu Sh. milioni 30.

Anasema, waliamua kujenga katika kata ya Kahumulo, kwa sababu asilimia kubwa ya kinamama wanaishi vijijini na anaendelea:

"Hadi sasa tuna jumla ya shilingi milioni 15, ambazo tumezipata kutoka Shirika la Kimataifa la Women First International Fund, lililoko nchini Marekani na shirika lisilo la kierikali linalotetea haki za wanawake (Kivulini) lenye makao yake jijini Mwanza."

### INAVYOJENGWA

Katika ujenzi, anafafaua kinamama ndio wanashiriki majukumu ya usaidizi kama kuchota maji, kuchanganya mchanga na saruji na kuwasadia mafundi, lengo ni kuwajengea hisia za umiliki halali, pale kitakapoanza uzalishaji.

"Waweze kuwa wabunifu zaidi katika bidhaa watakazozalisha. Lengo la Shirika la Mikono Yetu ni kukuza biashara za kinamama kwa kuzirasimisha," anaendelea Sophia.

### MCHANGO WA SIDO

Sophia anasema waliwapeleka wanawake 14 katika Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) mkoa wa Mwanza, wakafunzwe stadi za ujasiriamali, na usindikaji aina ya vyakula na matunda 130.

Anaeleza, Mikono Yetu inaamini mwanamke atakapomilikishwa rasilimali zalishi, anaondokana na ukatili katika jamii yake.

Meneja wa SIDO mkoani Mwanza, Bakari Songwe, anasema kiwanda tarajiwa kinakidhi viwango vya kiserikali, hivyo wataendelea kuwapa mafunzo na kuwaunganisha na taasisi mbalimbali za wanawake, wafanye na biashara yenye tija.

Katibu wa wanawake hao, Ankres Paulo, anasema wanatarajia kiwanda kitawaongezea kipato kupitia mazao ya mifugo, ikiwamo ng'ombe.

"Sengerema ina viwanda vingi ambavyo vinachakata mazao mbalimbali ya chakula, lakini hakuna kiwanda kinachochakata mazao ya mifugo, yakiwamo maziwa.

"Hali hiyo ilitukosesha fursa za kujiongezea kipato, maana wanawake wengi wa eneo hili tunajishughulisha na ufugaji," anasema.

Katibu huyo anasema katoka kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani wiki hii, waliendesha 'harambee' iliyowashirikisha wanufaika wote, wakapata Sh. 300,000, zitakazowasaidia kwenye ujenzi wa kiwanda.

"Kwetu sisi kiasi hicho ni kikubwa tutakuwa tunafanya hivyo mara kwa mara. Bado inahitajika shilingi milioni 10, ili ujenzi ukamilike.

"Tunawaomba wadau mbalimbali watakaoguswa watusaidie, Shirika la Mikono Yetu limetusaidia sana, sisi tunaendelea pia kujitoa katika shughuli mbalimbali za ujenzi kwa zaidi ya asilimia 70.

### WANUFAIKA

Wanufaika Secilia Medadi, Yunia Misana na Rachel Thomas, wana mtazamo kwanza kitakapokamilika kitasaidia kuwainua kiuchumi familia zao.

"Naamini uwapo wa bidhaa za aina mbalimbali sokoni ambazo tutazizalisha kiwandani, utasaidia kupata wageni wengi kutoka maeneo mbalimbali, ambao watasaidia kata yetu kuwa kitovu cha biashara ndani

INAENDELEA UK.14

BIASHARA

SHEREHE SIKU YA WANAWAKE

# Kutana na mwanamama dereva wa malori kuvuka mipaka nchi jirani

• Mwana: Karithi fani, magari, ajira ya mama

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

"WANAWAKE tusikate tamaa tunaweza... Nilikatishwa tamaa, lakini nilijipa moyo kwa kuwa nilijua nahitaji kuwa nani."

Ni miongoni mwa maneno anayoyatoa Modesta Charles, dereva wa malori ya wanawake nchini, ikiwa sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanamke Duniani yanayofanyika kila mwaka Machi 8.

Modesta, ni miongoni mwa wanawake shupavu wanaoendesha malori yanayofanya safari ndefu kutoka Dar es Salaam, hadi nchi jirani za Sudani, Burundi, Uganda na Kenya.

Anasema, mwanamke ana uwezo wa kufanya kazi yeyote na hapaswi kukatishwa tamaa, wala yeye kukata tamaa, kama ambavyo anasimulia safari yake ya maisha.



Modesta Charles, dereva wa malori mwanamama, akiwa na wenzake walipozungumza na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, alipotembelea maegesho ya malori katika eneo la Nala, jijini Dodoma.

### ALIVYOANZA & ANAVYOENDELEA

"Safari yangu kuwa dereva ilikuwa ngumu, lakini ni kitu ambacho kilikuwa kwenye damu tangu nikiwa mdogo. Nilipenda kuendesha magari tena makubwa," anasema.

Anasema kutokana na wazazi wake kufariki alilazimika kujisomesha kozi ya udereva katika Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) ili kufikia ndoto zake, akiwia na ufafanuzi:

"Nilikuwa mlinzi, hivyo nilijisomesha kwa fedha hizo na muda wangu, ulikuwa ni siku nikiwa nipo mapumziko kwenye kazi ya ulinzi ndio nikaenda chuo."

Dereva huyo anasema: "Wakati nakaribia kumaliza masomo yangu VETA, kuna watu walinifuata wakitaka niwe dereva wa basi nilikataa.

"Nikasema mimi nahitaji leseni ya kuendesha magari makubwa. Kuna watu walinisihi, lakini nilikataa nikasema sitaki kuendesha basi wala magari madogo, nataka lori."

Anaendelea na simulizi kwamba kwa sasa ana miaka sita kwenye kazi hiyo akiwa mwajiriwa. Anafafanua: "Miaka miwili kabla ya kuajiriwa niliitumia kufanya mafunzo kwa vitendo kwa kutembea kwenye magari haya makubwa, lakini kwa kuwa ni kazi niliyoipenda na ilikuwa kwenye moyo wangu nilipambana hadi nikafanikiwa."

> **Mimi ndio mama, nikatafakari nikaona nikimwacha mtaani atakaribikiwa hata matokeo yalipotoka hayakuwa mazuri.**

### KERO ZA BARABARANI

Analalamika kwamba, kilio chake kiko kwa askari wa barabarani ambao humkwaza katika utendaji wa kazi yake.

"Siwasemi vibaya, ila kuna vitu ambavyo vimekuwa kero na kuvunja moyo kwenye utendaji kazi. Kuna askari wengine waelewa, anakusimamisha na kukupa moyo.

"Askari unapaswa kunielekeza kwamba kitu hiki hupaswi kuwa nacho, lakini mwingine anakwambia unaendesha gari na kitu hiki, ngoja nikuonyeshe mwandikie faini huyo.

"Sasa kuna vitu vingine havina maana, kwa mfano askari wa Rwanda ukipatwa na shida au tairi imeisha, anakwambia nenda ila ukirudi na hii tairi usije njia hii na sitakuelewa," anaeleza kwa lugha ya mfano.

Hivi sasa mtazamo wake mkuu ni kwamba, serikali iangalie namna hatua ya kutoza faini za barabarani, kwani zingine zimekuwa kikwazo kwa madereva wenyeji.

### MWANAWE KARITHI

Jasiri huyo wa kike anaendeleza simulizi kwamba, ni aina ya uwajibikaji unaomsaidia kimaisha, hata amemudu kumsomesha mwanawe elimu hadi kidato cha nne, naye sasa amerithi taaluma hiyo akiwa dereva wa malori.

"Mwanangu nimemfundisha mwenyewe na ni dereva wa malori. Baba yake alifariki kwa ajali akiwa na miaka miwili. Nimehangaika naye kumpeleka shule, hadi sasa amekuwa dereva na tumeajiriwa kampuni moja," anasema.

Ilikuwaje hata mwana kurithi taaluma hiyo? Anajibu: "Mtoto wangu nadhani alikuwa naye anapenda tu, wakati nakabidhiwa gari alikuwa ndio amehitimu kidato cha nne na iliniuma sana kumuacha peke yake nyumbani.

"Mimi ndio mama, nikatafakari nikaona nikimwacha mtaani ataharibikiwa hata matokeo yalipotoka hayakuwa mazuri.

"Kwa hiyo, nilikuwa namchukua natembea naye kwenye gari hadi nchi mbalimbali, wakati wote nilikuwa naye. Kuna wakati nilikuwa namuona nikiwa nimeegesha gari, namkuta amewasha anataka kuiondoa.



Huyu ndiye Modesta Charles. **PICHA ZOTE: AUGUSTA NJOJI**

"Kuna siku hadi alilia akasema unanyima gari lako kuendesha. Kwa kweli nikamwendesha, alikuwa na kichwa kirahisi kufundishika hadi ofisini kwangu wakampenda wakamkabidhi gari. Tupo kampuni moja na hapa tunaongozana wote kwenda Sudani."

Saidi, mtoto wa Modesta anasema kitu kilichomsukuma kufuata nyayo za mama yake, ni kufurahishwa na namna mama yake alivyokuwa akiendesha gari.

Saidi anasema awali alidhani ni kitu rahisi kutokana na mama yake kuendesha gari, akahamasika nayo na kudokeza mwanzo wake ulivyokuwa.

"Akienda kuoga wakati mimi namsubiria tuondoke, mimi nachukua gari nahamisha na kuegesha sehemu nyingine. Alikuwa ananionya, akiniambia nisubiri muda bado sijajua kuendesha," anasimulia.

Anasema baada ya kufundishwa na mama yake kuendesha malori, alipelekwa katika Chuo cha Maendeleo ya Ufundi (VETA) kujifunza zaidi na akapata cheti kilichomwezesha kupata leseni.

"Namshukuru Mungu na mama yangu nimefikia ndoto zangu na nimeajiriwa," anasema.

### ASICHOKISAHAU

Modesta anaweka bayana mikasa iliyomgusa, kwamba: "Kuna wakati niliwahi kupata pancha eneo sio zuri katikati ya Arusha na Moshi. Tairi ya kubadili na vifaa vyote ninavyo, ila nilikuwa siwezi kubadili. Nilihitaji msaada, nilipata changamoto. Kwa kweli ilinilazimu kukaa zaidi ya saa tatu kuanzia saa nane usiku kila nikisimamisha gari zinapita.

"Kuna gari ilisimama, lakini dereva aliniporomoshea matusi, nadhani alifikiri labda ni 'dada wa kujiuza.' Iliniuma sana, sikuwa na jinsi. Nilikuwa na wasiwasi na nilikuwa na mzigo.

"Kuna 'kigari' kilipita awali na kikarudi nikasimamisha tena. Nikamkuta mzee nikamweleza naomba msaada mimi ni dereva, akasema ulinisimamisha nikakupita eeh! Nilifikiri ni mtu wa kujiuza. Alikubali kunisaidia yule babu hadi tukafunga tairi nyingine," anasema.

Anaongeza: "Sikukata tamaa, yule dereva aliyenitukana kuna siku nilimuona na akasema kuna siku ulinisimamisha, mimi nikamjibu nilishasahau na nilishakusamehe."

### WITO WAKE

Modesta anasema, kila kazi inahitaji kujiamini. Hivyo, wanawake wana uwezo wakufanya kazi zote zinazofanywa na wanaume.

"Mimi ninapotembea nchi za watu najifunza vitu vingine. Hapa nilipo, nipo na madereva wenzangu wanaume. Lakini, hawana tatizo na mimi kikubwa ni kutokata tamaa wananipa ushirikiano.

"Unachoweza kufanye mwanamke, usichukulie kwamba sijui watanionaje na wanaume watoe (wafute) fikra za kutufikiria vitu vibaya, wanawake tunafikiriwa vitu vibaya," anasema.

Pia, anawaasa wanawake wanaojiuza barabarani kuacha biashara hiyo haramu, kwa kuwa kazi zipo nyingi na mtu ana uwezo wa kufanya kuliko hilo la kujiuza.

"Kuna sehemu unapaki gari, anakuja mwanamke anagonga, anafikiri wewe ni mwanaume, ukifungua akajua ni mwanamke anashangaa au anakutukana matusi. Lakini, ni kitu ambacho ana uwezo wa kujifundisha na akaweza. Hii inaniuma sana," anasema mwanamama huyo jasiri.

### ENEO KOROFI?

Pamoja na hayo anasema serikali kwa kiwango kikubwa imekarabati miundombinu ya barabara huku akitaja eneo korofi barabarani kuwa ni eneo la kwenda mpaka wa Rwanda.

"Ajali nyingi zinatokea kwenye ile barabara. Nashukuru Mungu huwa napita, lakini ile barabara sio nzuri kutoka Nyakanazi hadi mpaka wa Rusumo, barabara ni korofi," anasema na kutoa kilio kwa serikali kutengeneza eneo hilo la barabara korofi.

Anataja mafanikio yake zaidi yaanzia kwenye kuzingatia sheria za usalama barabarani na kufuata alama zote zilizowekwa barabarani.

### KAULI KUU

Alipofungua kikao cha Bunge, Novemba mwaka jana, Rais John Magufuli, alisema serikali itahakikisha wamiliki wanatoa mikataba kwa madereva ili kuipa hadhi kazi hiyo.

"Jana Spika niliona unatambulisha madereva wanawake wa malori niwapongeze sana na wewe Spika na Naibu Spika, kwa kuanzia mnaweza kuendeshwa na dereva mwanamke.

"Katika suala la madereva inawezekana katika bunge hili ikatungwa sheria mahsusi ya kuwalinda madereva wetu wa nchi," anasema.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Mheshimiwa Rais kero si maji tu, pia umeme






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**jkulangwa@yahoo.com**

KAMA ilivyo kawaida yake ya kutomung'unya maneno na imani yake ya ukweli kuwa upenzi wa Mungu, hivi karibuni Rais John Magufuli aliitolea uvivu Wizara ya Maji, kwa ilivyomsumbua katika miaka mitano iliyopita katika uongozi wake.

Kubwa, ni kwamba wizara hiyo muhimu kwa ustawi wa jamii, ilikwamisha kukamilika miradi iliyopangwa kutekelezwa.

Ni hali iliyomlazimu Rais kubadilisha mawaziri wenye dhamana ya maji kila mara, kwa lengo la kuhakikisha miradi hiyo mikubwa na muhimu inakamilika na bado kukawapo kupwaya.

Sasa akamtaka waziri wa sasa kung'ata fupa hilo.

Rais Magufuli ni mtu wa miradi, ndiyo sababu anafuatilia kupitia wasaidizi wake, lakini naye akiwa pembeni akiangalia kwa ukaribu, utekelezaji wa miradi hiyo inayotumia fedha kodi za Watanzania.

Inaumiza kuona miradi iliyopangwa ikisuasua, huku waliopewa dhamana ya kuisimamia wakiendelea kulipwa mishahara na stahiki zao, kana kwamba hawajui jinsi wananchi wanavyoumia kwa ama kukosa majisafi na salama au kuyapata kutoka masafa marefu.

Wakati Rais akilia na wizara hiyo ya maji, kwa upande wa pili, wananchi nao wanalia na wizara zingine, ikiwamo ya Nishati, ambayo inasimamia umeme, kutokana na kukosa ufanisi katika medani hiyo ya huduma.

Si siri, kwamba Waziri wa Nishati, Medard Kalemani ni mchapa kazi na mfuatiliaji wa karibu ndani ya wizara hiyo na imedhihirisha jinsi anavyochanja mbuga, milima na mabonde, kuhakikisha kila kona ya nchi inapata umeme, lakini ni dhahiri kuna watendaji wake huko chini wanamwangusha.

Umeme umekuwa ukikatika kila mara katika sehemu mbalimbali za nchi, hususan mijini, ambako ndiko kwenye viwanda na kusababisha uzalishaji unakwama kama si kusuasua. Hivyo, kunashuhudiwa hasara kwa wenye viwanda, taasisi na taifa.

Watumiaji wengi majumbani wamekuwa wakikumbana na adha hiyo ya kukatika umeme na kurudi na kusababisha baadhi ya vifaa vyao kuharibika.

Wanakosa namna ya kufidiwa, kutokana na mlolongo uliopo katika kudai hata kupata fidia na mwishowe kumwachia Mungu.

Umeme umekuwa ukikatika kwa sababu za nje ya uwezo wa wasimamizi, lakini wakati mwingine ndani ya uwezo, kwa sababu ambazo wakati mwingine zinaonekana kuwa za kizembe.

Mathalan, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kutoa sababu za kukata matawi ya miti, nguzo kuoza, kunguru kukanyaga nyaya, kurekebisha transfoma, na kadhalika. Hizo ni sababu za kila siku na kila mara.

Unajiuliza hiyo miti huota kila siku na kama iko kwenye njia za nyaya kwa nini ising'olewe, kwanini pia nyaya zisipitishwe ardhini kama alivyopata kushauriwa huko nyuma na waliowahi kuisimamia wizara hiyo? Hivi nguzo za zege zitasimikwa lini?

Huko tuendako kuna uhakika wa kuwa na umeme mwingi kutoka Bwawa la Nyerere, lakini kama hakutakuwa na usimamizi, athari chanya za bwawa hilo hatutaziona, umeme utakatika kwa sababu hizo hizo za kijima. Alamsiki!

UCHUMI

# Bosi TPDC achambua uchumi gesi unavyokaribisha Tanzania Viwanda

• Aeleza ilivyo safari ya 'baibai mkaa' • Wajiolojia nyumbani wafanya makuu • Mkakati mbioni kukamata soko EAC

**Na Anthony Gervas,** MWANZA



Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dk. James Mataragio. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

GESI ni malighafi inayozalishwa nchini kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Hata hivyo, gesi asilia inatajwa kutumia kiwango kidogo, tofauti na mitungi kutoka nje ambayo ina gharama ya ziada.

Umma mkubwa hadi sasa unaangukia nafuu ya maisha, baada ya kupatikana gesi nchini. Ni kinyume na zamani, walipolazimika kutumia nyenzo mkaa unaotajwa sasa kuwa mzigo wa gharama kubwa, hasa kwa wananchi maskini wanaohemea zaidi kuni.

Zipo familia maskini mijini na vijijini, bado zinalazimika kutumia kuni badala ya gesi au mkaa. Msingi wa teknolojia ya gesi, imekuja na tija ya utendaji, huku ikipunguza gharama za maisha kuondokana na mkaa, kuni na mafuta ya taa.

**UGUNDUZI WA GESI**

Dk. James Mataragio, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), ana simulizi zaidi kuhusu ugunduzi za gesi, uzalishaji wake, hali kadhalika kwa mafuta nchini na tija yake kiuchumi.

Bosi huyo wa TPDC, anasema ugunduzi za gesi nchini mara ya kwanza ulifanyika mwaka 1974 na mara ya pili ni mwaka 1982 huko katika visiwa vya Songosongo.

Dk. Mataragio anasema, mara ya kwanza ilikuwa kazi ya wataalamu wa jiolojia wa ndani na nje ya nchi, lakini awamu pili ulikuwa ubunifu wa wajiolojia wa nyumbani.

**UZALISHAJI GESI**

Anabainisha kuwa, uzalishaji wa gesi nchini umefikia kiasi cha futi za ujazo bilioni 288 mwaka 2020, kutoka kiasi cha futi za ujazo bilioni 163 mwaka za 2014.

Mkuu huyo wa TPFC anaitaja hiyo kuwa mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za taasisi hiyo, sekta ya mafuta na gesi na kwa mujibu wa Dk. Mataragio, ikiwa uchakataji wa gesi kati ya mwaka 2010 hadi 2014 ulikuwa futi za ujazo bilioni 162.

Hata hivyo, kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 uliongezeka na kufikia kiasi futi za ujazo bilioni 287. Hiyo inaenda sambamba na uwezo wa mitambo ya kuchataka gesi kutoka 2014 uliongeza zaidi ya mara tatu na nusu. Upande wa mabomba yameongezeka hadi kufikia mwaka jana ulikuwa urefu wa kilomita 810, kutoka kilomita 259 za mwaka 2014.

Wakati Dk. Mataragio anajivuna gesi kuanzia mwaka 2015 ilichangia ongezeko la megawatt 531 sawa na asilimia 147, kwa maana ya kufikia megawati 892, hali inayofanya kuokolewa fedha Sh. trilioni 17, kwa matumizi ya gesi badala ya mafuta, ikiwamo katika magari.

**MATUMIZI NA MAHITAJI**

"Ajira rasmi katika sekta ya utafutaji na uendelezaji mafuta na gesi mwaka 2014 rasilimali watu ilikuwa 575 na kufikia mwaka 2020 imefikia 820," anasema Dk. Mataragio.

Anasema, vilevile kuna kiasi kikubwa cha gesi kilichogunduliwa na bado hakijaendelezwa, ikiwa ni futi za ujazo trilioni 40, ambayo ipo baharini, hivyo kazi kubwa inayokusudiwa na serikali ni kujiandaa kuendeleza na kuivuna.

Mkuu wa TPDC, anasema kuna mradi mkubwa unaokusudiwa kujengwa eneo la Likong'o Lindi, ambako utakuwa unabadilisha gesi itakayovunwa baharini katika hali ya mvuke na kufanywa kimiminika. Anasema lengo kuu la huduma hiyo kitaalamu, ni kuiwezesha isafirishwe katika nchi jirani, huku asilimia kubwa ikibakishwa kwa matumizi nchini.

Dk. Mataragio anasema mpango ulioko ni kwa serikali kuingia makubaliano ya kuuza na kusambaza gesi katika nchi jirani kama vile Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia Congo (DRC), Uganda, Zambia na Burundi,

Anasema, hiyo inatokana na mahitaji makubwa ya gesi katika maeneo hayo kutokana na kukua uchumi wake, hivyo zinahitaji nishati zaidi. Pia anasema hadi sasa asilimia 60 ya umeme wote nchini unazalishwa na gesi na katika biashara hii sasa kuna kasi kubwa ya mahitaji ya nishati gesi.

**VITUO VYA GESI**

Dk. Mataragio anasema matarajio yaliyoko, ni kujengwa vituo vitano vya kushindilia gesi mkoani Dar-es Salaam na vituo vya kujazia gesi kwenye magari na kusafirishia kwenda kwenye mikoa mbalimbali kama vile Dodoma, Tanga, Morogoro na Mwanza.

Anasema, vilevile gesi hiyo itasambazwa kwenye migodini kwenye maeneo kama ya jumuiya za wachimbaji wadogo wa madini, viwandani, kukitarajiwa kuwapo mitambo mikubwa ya kugeuza gesi kimiminika, ili isafirishwe katika hali ya kimiminika.

Makusudio mengine anayoyataja ni kusudio la maeneo yote ya mbali na bomba la mafuta, kutajengwa vituo vya kushindilia gesi maarufu 'CMG' ili kuweza kusafirisha katika maeneo yasiyokuwa na miundombinu.

Anasema, ni matumizi yatakayoanza mwaka huu katika vituo vitakavyowekwa kwenye maeneo mbalimbali mikoani, pamoja na maeneo ya safari za treni ya mwendo kasi zitakapoanza.

**PESA ZILIVYOOKOLEWA**

Mkurugenzi wa TPDC, anasema serikali imeokoa kiasi cha Sh. trilioni 33 kutokana na kutumika mbadala wa gesi asilia, pesa zilizoelekezwa katika matumizi mengine ya kiuchumi wa kitaifa.

Pia anasema imeweza kulipa takribani Sh. bilioni 600 za kodi mbalimbali zitokanazo na mauzo ya gesi asilia na wakati huo huo TPDC imerejea katika biashara ya mafuta na bidhaa zake kupitia kampuni tanzu iliyoiunda ya TANOIL.

Aidha, anaeleza hadi sasa imefanikiwa kutwaa maeneo baadhi nchini ikiwamo katika mikoa Tanga, Dodoma na Dar es Salaam, lengo lililopo ni kujenga maghala ya kuhifadhi mafuta ya kimkakati.

Pia anataja mikakati kuwa ndani ya miaka mitano ijayo, serikali inatarajia kujenga vituo vya mafuta 100 nchi nzima kwa kushirikiana na halmashauri mbalimbali na sekta binafsi.

Kwa mujibu wa Dk. Mataragio, mtazamo ulioko ni kuifanya Tanzania kituo kikuu cha kuhudumia nchi za Afrika Mashariki na Kati na kukuza uchumi wa viwanda vya ndani, kuongeza fursa za ajira na kuchangia pato la taifa.

## Kiwanda rasmi cha kinamama wa Sengerema, kila kitu ni wao

**INATOKA UK.11**

ya wilaya hii," anasema Secilia.

Rachel, ana mtazamo kiwanda kitamsaidia kusindika mazao yake ya chakula kutoka shambani yaliyokuwa yanaharibika.

"Huwa najishughulisha na kilimo cha nyanya. Kama unavyojua zao hilo, linawahi kuharibika. Kabla sijapata mafunzo ya usindikaji kutoka SIDO, nilikuwa nikikosa wateja, nyanya nyingi zilikuwa zinaharibika au inabidi nizigawe kwa majirani.

"Tangu nimepata mafunzo nimeanza kusindika, shauku yangu ni kuona kiwanda kinaanza ili nifanye kazi hiyo kwa tija zaidi," anasema.

Yunia Misana, anasema kiwanda tarajiwa kitawakomboa wanawake wanaojishughulisha na kilimo katika kata hiyo, kwa sababu awali walikosa utaalamu wa kusindika.

**SERIKALI MTAA**

Diwani wa Kata ya Kahumulo, Fortunatus Nzwagi, anaunangalia mradi huo katika sura ya chachu ya maendeleo kwa wakazi wake, kwani jamii sasa itawezeshwa kupitia mwanamke anayeinuka.

Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Kepha Chima, anaomba wadau na asasi zingine kwenda kuwekeza katika eneo hilo, kutokana na uhalisia wa rutuba yake.



Wajenzi kinamama wakiwa kazini. **PICHA: CLAR A MATIMO**





# Waomba kasi maboresho sheria usalama barabarani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WADAU wa masuala ya usalama barabarani wameiomba serikali kuharakisha mchakato wa marekebisho ya upungufu yalipo kwenye Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973, ili iendane na wakati ulipo.

Hayo yalibainisha jana na Mwenyekiti Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali la Mwanza Youth and Children Network (MYCN), linalotekeleza mradi wa usalama barabarani kwa watoto, Brightius Titus, katika kikao cha kujadili usalama barabarani kwa watoto.

Aalisema kikao hicho cha kujadili masuala ya usalama barabarani kwa watoto kilihusisha wizara tano pamoja na ofisi ya mwanasheria mkuu wa serikali.

Alisema katika kikao hicho wameangalia upungufu uliyopo katika Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973.

Alisema moja kati ya upungufu huo ni uvaaji wa mikanda, ambapo sheria inamtaka abiria wa mbele pamoja na dereva ndiyo wavae mikanda, lakini kwa wengine ipo kimya.

"Lakini upungufu mwingine ni namna gani sheria hii inamlinda mtoto kwani katika kifungu cha 39 sheria hii inatambua watoto wawili wa chini ya umri wa miaka 12, kuwa ni abiria mmoja," alisema Titus.

Upungufu mwingine alisema ni matumizi ya mikanda katika usafiri wa umma ambapo inatakiwa kuwapo kwa mikanda ambayo inaweza kutumika na watoto katika mabasi na viti maalum.

Pia alisema sheria hiyo imekuwa kimya kwa watumiaji wa usafiri wa pikipiki maarufu kama bodaboda, ambapo uvaaji wa kofia ngumu kwa abiria haisemi chochote.

"Pamoja na kuwa katika sheria zile la LATRA kuelekeza abiria wa bodaboada anatakiwa kuvaa kofia ngumu, lakini sheria mama yenyewe imekaa kimya hivyo yanahitajika marekesho ya haraka ili kupunguza ajali," alisema Titus.

Vile vile, alisema katika magari ya shule sheria inasema kila abiria awe na kiti chake, lakini sheria hiyo inatambua abiria kuwa ni mtu mzima kuanzia miaka 18.

"Hii ndiyo ambayo inawalinda wamiliki wa shule ambao wanasimamisha watoto au kujaza kupita kiasi kwakua tu sheria inatambua abiria kuwa ni mtu mwenye umri kuanzia miaka 18," aliongeza.

Naye CPL Martin Mangu, kutoka Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Dodoma, alisema ipo haja elimu ya usalama barabarani kuanza kufundishwa katika shule.

Alisema, kutokana na umuhimu wa elimu hiyo, kunahitajika kuandaliwa kwa mitaala ambayo itaanza kufundishwa katika shule kuanzia ngazi ya darasa la awali ili kuondokana na ajali.

Kwa mujibu wa takwimu za mashirika yanayojihusika na masuala ya usalama barabarani (Global Road Safety Partnership), watu milioni 1.35 hufariki dunia kutokana na ajali kila mwaka, huku idadi kubwa ikiwa ni wale mwenye umri wa miaka 5 hadi 29.



Mbunge wa Jimbo la Kijini Zanzibar, Yahaya Ali Khamisi, akichangia mada kwenye kikao cha Kamati ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo, walipokutana na Uongozi wa Wizara ya Maji, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Viwanda wajadili mikakati utekelezaji bajeti

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, amekutana na kufanya kikao na menejimenti, wakuu wa idara, vitengo na wakuu wa taasisi zilizo chini ya wizara hiyo kwa lengo la kuweka mikakati na kujadili utekelezaji wa bajeti katika kufikia malengo.

Akifungua kikao hicho cha siku mbili, Waziri Mwambe alizitaka kila taasisi kuhakikisha zinafanya kazi kwa weledi na ubunifu mkubwa na kwamba katika bajeti yake kila taasisi ilenge katika miradi ya maendeleo na ipewe kipaumbele katika mipango ya utekelezaji wake.

"Nataka kila taasisi ihakikishe katika bajeti yake inalenga miradi ya maendeleo itakayosaidia kukua kwa taasisi, pia kila taasisi ipunguze kwa kiasi kikubwa matumizi yasiyo ya lazima tunataka bajeti ilete tija," alisema Mwambe.

Aidha, alizitaka taasisi katika bajeti yake zilenge vipaumbele vichache ambavyo vitatekelezeka na sio kuweka vingi na bajeti ikawa haitoshi na fedha kutawanywa katika sehemu mbalimbali, hivyo mwisho hakuna matokeo katika utekelezaji wake.

Alizitaka taasisi kufanya kazi kiubunifu ambapo amebainisha kuwa Tanzania ni nchi ambayo imejaliwa kuwa na fursa nyingi lakini bado hazijaleta tija kwa jamii na kuwa ni wajibu wa taasisi kuwa wabunifu wa nini kifanyike.

"Ukiangalia katika kilimo hasa vijijini miaka nenda rudi tunatumia majembe ya mkono hiyo tija itapatikana sangapi na taasisi za utafiti zipo tu, kabla ya kuondoka katika hiki kiti nataka nizindue jembe lililobuniwa na CAMARTEC linaloleta mapinduzi," alisema.

"Hatuna kiwanda cha kutengeneza nguo lakini malighafi zipo na kila siku yanasafirishwa marobota mengi na mwisho wa siku tunauziwa nguo, wakati uwezo tunao wa kuwa na viwanda hapa nchini nataka hili lifanyiwe kazi haraka sababu nguvu kazi tunayo," alisema.

Alitaka Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE) kuja na mikakati ya kuhakikisha wanaweka mazingira mazuri ya biashara hasa kwa wajasiriamali katika halmashauri zote ili kuwaendeleza wafanyabiashara hao kukua.

Pia aliitaka TANTRADE kuwa na mikataba ya mazao ya kibiashara kama korosho badala ya kusubiri minada ambayo sio uhakika huku akitaka kuja na teknolojia inayofaa ili kuhakikisha korosho zinabanguliwa na sio kuuza ghafi.

Aidha, alikitaka Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kubadili mtazamo wake na kuanza kutoa elimu itakayomuwezesha mwanafunzi anapomaliza masomo kwenda kuanzisha biashara na sio kuwa wasimamizi wa biashara.

Kadhalika, aliitaka Tume ya Ushindani kufanya kazi kwa ubunifu na si kwa mazoea ili kuhakikisha wawekezaji wanawekewa mazingira mazuri.

"Tume ya ushindani msiwasumbue wenye viwanda kuna njia nyingi badala ya kufunga biashara yake na huyo mwenye kiwanda kuona namna ya kumaliza mapungufu hayo sio kumfungia kiwanda chake," alisema.

Naye Naibu wa Waziri wa Wizara hiyo, Exaud Kigahe, alikemea vitendo vya uchepushaji wa fedha za miradi ambapo taasisi nyingi zimekuwa zikitumia fedha kutekeleza miradi ambayo haikukusudiwa tangu awali.

# Wizara Kilimo, JKT kujikita kulima mahindi ya njano

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, amesema wizara hiyo itakaa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa ajili ya kuweka mikakati ya namna watakavyozalisha mahindi ya njano kwa lengo la kupeleka nchini Misri ambapo soko limepatikana.

Alisema hayo alipokuwa akizungumza hivi karibuni wakati wa kukitia saini kwenye mkataba wa ushirikiano uliolenga kufanya Jeshi hilo kuzalisha kwa tija na kufikia kilimo biashara.

Kusaya alisema Wizara hiyo inaitegemea JKT kwani ndio taasisi ya umma iliyojikita zaidi katika miradi ya kilimo.

"Miongoni mwa shughuli tutakazozifanya katika mashirikiano haya ni kubadilishana taarifa na upatikanaji wa masoko yaliyofikiwa kwa haraka.

"Kwa mfano hivi majuzi wizara tulitembelewa na ugeni kutoka Misri, ambao ulihitaji kupata mahindi ya njano tani milioni moja, na sisi sasa tunatazama ndani ya taasisi za umma na tunaona JKT... hatuwezi kukosa mahindi haya,hivyo katika mashirikiano yetu haya inabidi tuangalie ni kwa namna gani tunaweza kulima mahindi haya kwani soko tayari lipo," alisema Kusaya.

Vile vile, alisema kwa kushirikiana na JKT, wataangalia katika kuzishirikisha taasisi binafsi katika uzalishaji wa mahindi hayo.

"Kwa hiyo tunaamini kuwa na uhusiano haya tunaweza kufika sehemu tukapata haya mahindi," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Kusaya, kwa sasa Wamisri wanahitaji tani 25, kwa mwezi, na kuwa kama uzalishaji tutakuwa mzuri zaidi wataongeza hadi kufikia tani 75,000.

"Sasa soko lipo changamoto ni kwetu sisi watanzania tushirikiane kati ya taasisi za umma na binafsi kuhakikisha suala hilo linafanikiwa kwa lengo zina la kuinua uchumi wa Taifa letu," alisema.

Pia Kusaya alisema uhusiano wao wataifanya JKT kuzalisha zaidi huku ikiwa na uhakika wa soko.

Alisema suala la utafutaji wa masoko watalifanya kwa pamoja na JKT kuhakikisha kabla ya kuzalisha zao fulani kuwe na soko la uhakika la kukuza zao hilo.

"Hilo ni moja kati ya maeneo ya ushirikiano ambalo tutakwenda kujikita kwa maana kwamba baada ya JKT kuzalisha mazo hayo yatahitaji soko, sasa kwa pamoja sisi na JKT tutajenga mahusiano mazuri ya kutafuta masoko ya mazao hayo.

Alisema eneo lingine katika mahusiano hayo ni kufanya huduma za usimamizi wa mazao baada ya mavuno na uongezaji wa thamani ambao ni kufanya utafiti wa mradi ya maendeleo ya pamoja.

"Tunaweza kuangalia eneo la kuongeza thamani kwamba ifike wakati JKT tukishazalisha tusiuze mpunga bali tuuze mchele, na hapo tutapata vitu vingi likiwamo kuzalisha ajira, pumba za chakula cha kuku, chenga za mchele wa vitumbua, lakini pia tutapata malighafi uchomaji matofali na mbolea."





## TRA yawaonya wafanyabiashara bidhaa magendo

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

OFISA Mfawidhi wa Forodha wa Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa wa Mbeya, amewataka wafanyabiashara mkoani humo kufuata kanuni na taratibu za uingizwaji wa magari kupitia forodha zilizopo kwenye mipaka ya nchi, badala ya kutumia njia za magendo ambazo zinaikosesha serikali mapato.

Robert Nyoni alitoa rai hiyo jana wakati wa hafla ya kukabidhi gari kwa Jeshi la Polisi ambalo limetolewa na mamlaka hiyo baada ya kutaifisha.

Nyoni alisema mfanyabiashara yeyote atayekamatwa anavusha bidhaa yakiwamo magari kwa njia ya magendo, adhabu yake siyo kukamatwa na kulipa faini tu, bali ni mali zake kutaifishwa.

Alisema kwa kawaida mali hizo zikikamatwa, zinagawiwa kwa taasisi za umma au binafsi ambazo zimewasilisha maombi kwa TRA juu ya vitu wanavyovihitaji.

"TRA tuna utaratibu endapo tumelikamata gari ambalo aidha liliingia nchini bila kibali kwa maana ya kutolipia mapato wala kulisajili, tunalitaifisha na kugawa kwa taasisi zenye uhitaji," alisema Nyoni.

Akikabidhi gari hilo lenye thamani ya Sh. milioni 17, Mbunge wa Mbeya Mjini na Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema litasaidia kurahisisha utendaji kazi.

Alisema Jeshi la Polisi linakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi ikiwamo magari, hivyo msaada huo utasaidia kutimiza majukumu yao kwa wakati katika kuwalinda raia na mali zao.

Dk. Tulia aliongeza kuwa bado Jeshi la Polisi linahitaji uboreshaji wa miundombinu ya makazi ya jeshi hilo ambapo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, nyumba sita tayari zimejengwa huku nyingine nne zikitarajiwa kukamilika hivi karibuni.

# Hospitali yazibeba gharama kutibu figo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ASILIMIA 75 ya wananchi wanaougua magonjwa ya figo na kutakiwa kupata tiba ya kusafishwa damu katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, hawana uwezo wa kulipia matibabu hayo kutokana na huduma hiyo kutolewa kwa gharama kubwa.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Figo katika hospitali hiyo, Dk. Octavian Kasanga, mbele ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, aliyezuru wodi ya wagonjwa wa figo hospitalini huko.

Alisema kati ya wagonjwa wanne wenye matatizo ya figo, watatu hawana uwezo wa kumudu gharama za matibabu na kwamba inapotokea hali hiyo, baadhi yao wanalazimika kuchangia na wengine kupata msamaha.

"Serikali imeandaa mazingira mazuri katika kuwahudumia wenye matatizo ya figo ndiyo maana tunapokea wagonjwa kutoka maeneo mbalimbali ya mikoa ya nyanda za juu kusini huduma zetu ni nzuri kuna vifaa vya kutosha na wataalamu waliobobea katika ugonjwa wa figo," alisema Dk. Kasanga.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, alisema pamoja gharama kubwa, uwepo wa huduma hiyo kwenye hospitali yake umesaidia wananchi kuipata karibu na makazi yao.

Alisema kuanzishwa kwa huduma za usafishaji wa figo katika hospitali hiyo, kumesaidia wananchi wa ukanda wa Nyanda za Juu Kusini kuzipata kwa wakati hasa kwa wale wanaotakiwa kusafisha figo angalau mara tatu kwa wiki.

Alisema huduma hiyo awali ilikuwa inatolewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili jijini Dar es Salaam, hivyo wananchi kutumia gharama kubwa kusafiri na kupata matibabu na wengine kushindwa kumudu gharama.

Daktari Bingwa wa Figo kutoka Hospitali ya Rufani ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma, Dk. Linda Ezekiel, alisema mgonjwa mmoja wa figo kwa kipindi cha mwaka mmoja anachangia gharama za matibabu zaidi ya Sh. milioni 40.

Aliongeza kuwa gharama za matibabu ya figo ni kubwa, hivyo aliwashauri wananchi kuzingatia ulaji sahihi wa vyakula, kufanya mazoezi ili kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza ambayo kwa kiasi kikubwa yanachangia tatizo la figo.

Akizungumzia mpango wa serikali kupunguza gharama za matibabu ya figo nchini, Waziri Gwajima alisema wameongeza huduma za kibingwa katika hospitali zote za rufani za kanda kuhakikisha zinatoa huduma ya usafishaji damu.

Alisema serikali imelenga kuziwezesha hospitali zote za rufani za mikoa nchini kutoa huduma za matibabu ya figo ikiwamo usafishaji wa figo ifikapo mwaka 2025.

Dk. Gwajima alisema serikali inafanya mapinduzi katika utoaji huduma ya matibabu ya figo kwa kuhakikisha mashine vitendanishi na vifaa vyote vinatakiwa vipatikane kwa gharama nafuu kuanzia zinakonunuliwa.

Alisema Bohari ya Dawa (MSD) tayari imekamilisha mpango kwa kusambaza mashine kutoka vyanzo nafuu na vitendea kazi vingine kutoka kwenye gharama ya kuanzia Sh. 30,000 hadi 60,000 na kwamba wizara inawasilisha muswada kuhakikisha wananchi wote wanakatiwa bima ya afya.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (katikati), akitoa pole kwa wananchi wa Kata ya Iyela, jijini Mbeya juzi, alipohudhuria shughuli ya mazishi ya mlinzi wa aliyekuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani, Bethuel Mila, aliyeuawa kikatili kwa kupigwa nondo na watu zaidi ya watano. Kulia kwake ni Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# RC alibana jiji mpango watoto wenye ulemavu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ametoa wiki tatu kwa uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuandaa mpango kazi utakaoainisha mahitaji mbalimbali ya watoto wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi Itiji ili serikali na wadau waisaidie.

Chalamila alitoa agizo hilo juzi alipozuru katika shule hiyo na kuangalia mazingira wanayosoma watoto wenye mahitaji maalum.

Kutokana na mazingira ya shule hiyo kutokuwa rafiki kwa kundi hilo, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na vyoo kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum, vifaa vya kujifunzia na eneo la michezo, alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, kwa kushirikiana na viongozi wenzake, kuandaa andiko ambalo litabainisha mahitaji yote ya muhimu kwa ajili ya kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum ili wasome kwa furaha.

"Ninawapongeza walimu kwa kazi nzuri mnayoifanya. Licha ya kufundisha kwenye mazingira magumu, mnapambana. Nimeona hakuna vyoo rafiki kwa watoto wenye mahitaji maalum, hapa wanatumia vya watoto wa kawaida. Lazima tushirikishe wadau kusaidia ujenzi huo," alisema Chalamila.

Kiongozi huyo alisema Shule ya Msingi Itiji ni miongoni mwa shule jumuishi ambao zinakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwamo miundombinu ya madarasa, vyoo, vitendea kazi na maeneo ya michezo.

Alishauri uongozi wa shule hiyo kufanya mawasiliano na walimu wa Shule ya Msingi Makalala iliyoko mjini Mufindi mkoani Iringa kujifunza namna walivyofanikiwa kuendesha shule hiyo yenye watoto wenye mahitaji maalum na kawaida.

Aliwaagiza viongozi wa jiji kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa bweni ili kuwasaidia watoto wenye ulemavu ambao wanatoka mbali, kukaa shuleni na kupunguza tatizo la utoro na madhara mengine ambayo yanaweza kutokea wakati wa kwenda na kutosha shuleni.

Kutokana na mazingira hayo, Chalamila alitoa msaada wa fedha Sh. milioni moja kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vyoo huku akiwaagiza viongozi wengine kuchangia ili kukamilisha ujenzi wa matundu sita ya vyoo na hosteli kwa ajili ya watoto hao.

Akizungumzia tatizo la uhaba wa matundu ya vyoo kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum, Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Jerome Kayange, alisema jumla ya watoto 92 wenye mahitaji maalum kati ya watoto 574 waliopo shuleni hapo.

Alisema shule hiyo ni jumuishi na kwamba miundombinu iliyopo ni rafiki kwa watoto wa kawaida lakini siyo rafiki kwa wenye ulemavu.

Alisema shule hiyo ina walimu 20 (wanawake 17) na kati yao, walimu tisa wakifundisha watoto wenye mahitaji maalum.

Mwalimu anayefundisha watoto wenye matatizo ya akili, Clement Nyabumbwe, alisema vifaa vya kujifunzia havikidhi mahitaji kwa kuwa watoto wenye shida hiyo muda mwingi wanahitaji shughuli za kufanya na michezo mbalimbali.





Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Gavana wa Mombasa Kenya, Ali Hassan Joho (wa pili kushoto), Ikulu jijini Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU**

# W/biashara wa Kenya wakaribishwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewakaribisha wafanyabiashara wa Kenya kuwekeza na kufanya biashara Zanzibar hasa ikizingatiwa kwamba pande mbili hizo zina historia katika sekta ya biashara.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu alipokutana na kufanya mazungumzo na Gavana wa Mombasa, Ali Hassan Joho, akiwa amefuatana na ujumbe wa wafanyabiashara kutoka Mombasa, ambao walionesha nia ya kufanya biashara kati ya Mombasa na Zanzibar.

Rais Dk. Mwinyi alimweleza Gavana Joho kwamba Serikali ya Zanzibar imeweka mazingira mazuri kwa wawekezaji na wafanyabiashara, ambao wana lengo la kuekeza na kufanya biashara Zanzibar.

Alisisitiza kwamba serikali imeweka mikakati maalum katika kuwavutia wafanyabiashara pamoja na wawekezaji ambapo kwa kupitia Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), itaendelea kuweka mazingira mazuri.

Alieleza kwamba pande zote mbili za visiwa vya Zanzibar hatua za makusudi zinachukuliwa kuhakikisha shughuli za uwekezaji pamoja na kuwavutia wafanyabiashara zinatekelezwa kwa Unguja na Pemba.

Alisema serikali imeweka milango wazi kwa wawekezaji na wafanyabiashara kwenda kufanya shughuli zao katika sekta wanayoitaka na kuwa sera, sheria na taratibu za kuhakikisha biashara kati ya pande mbili hizo zinafanyika vizuri.

Alieleza kuwa kuvutiwa na nia ya wafanyabiashara wa Mombasa kutaka kufanya biashara ya sukari inayotoka katika Kiwanda cha Mahonda Zanzibar na kupeleka katika Soko la Mombasa na kuwa hatua hiyo itapanua soko la bidhaa hiyo.

Rais Dk. Mwinyi alimpongeza Gavana Joho kwa kufika Zanzibar akiwa ameambatana na wafanyabiashara na kumweleza kwamba Zanzibar iko tayari kuwakaribisha ndugu zao wa Mombasa kufanyabiashara nao.

"Tanzania na Kenya zina uhusiano wa muda mrefu hasa kwa upande wa Mombasa na Zanzibar, pande mbili hizo zina historia ya biashara," alisema.

Naye Gavana Joho alisema lengo la safari yake ya kuitembelea Zanzibar akiwa na wafanyabiashara wa Mombasa ni kufanyabiashara kati ya pande mbili hizo.

Alisema wafanyabiashara hao wako tayari kufanyabiashara na Zanzibar na baadhi yao wameshaanza mchakato wa biashara zao kwa kuamini kwamba soko la biashara Zanzibar lipo.

Gavana Joho alimweleza Rais Dk. Mwinyi kwamba historia inaonyeshwa kwamba Zanzibar na Mombasa zina uhusiano na ushirikiano wa miaka mingi, hivyo, ni vyema ukaimarishwa.

Kuhusu sekta ya utalii, alisema ni vyema pakawapo ushirikiano ili kila upande uzidi kupanua wigo kwa mwenzake kwa azma ya kukuza sekta hiyo.

## Ngoma za vigodoro zapigwa marufuku

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, amepiga marufuku upigwaji wa ngoma za vigodoro na khanga moja kwa kuwa ngoma hizo sio utamaduni wa Wazanzibari.

Alitangaza marufuku hiyo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari juu ya alivyojipanga katika miaka mitano ijayo kuhusu mwelekeo wa Serikali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja katika awamu ya nane.

Alisema kumekuwa na kawaida kwa wananchi kutoka katika sehemu mbalimbali Zanzibar kufika katika mkoa huo kucheza ngoma hizo na kuvunja mila na tamaduni zilizopo.

"Sio ruhusa kwa wakazi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja na wananchi kutoka sehemu nyingine kuja kupiga ngoma na kucheza... na ngoma hizo zimekosa maadili," alisema Ayoub. Aidha, alisema serikali imelenga katika sekta ya utalii na mkoa huo una vivutio vingi ikiwamo hoteli na migahawa mikubwa ambapo wananchi watapata fursa kujua sehemu hizo Pia alisema jinsi mkoa ulivyolenga mambo mbalimbali yanayohusu jamii ikiwamo kilimo, mifugo, maji na salama, elimu, afya pamoja na michezo.

Kadhalika, alisema serikali ya mkoa huo imelenga katika kuimarisha viwanda vya kusindika vyakula kama mananasi na mboga ili wakulima waepukane na hasara katika mazao wanayolima kila msimu.

Vilevile, alisema atahakikisha anadhibiti vitendo vya udhalilishaji, dawa za kulevya na rushwa, kwa kuwa vinarudisha nyuma maendeleo ya Taifa.

# Waziri apiga 'stop' ujenzi wa kiwanda nyaya za umeme

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salum, amemwagiza Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mazingira Zanzibar (ZEMA), kuzuia ujenzi unaotarajiwa kuanza wa kiwanda cha kuzalisha nyaya za umeme kutoka Kampuni ya ZANTEXAS LIMITED.

Hatua hiyo inafuatia kutokuwapo kwa taarifa zozote kutoka kampuni hiyo na Mamlaka ya Mazingira, jambo ambalo ni kinyume cha sheria na taratibu za kuanzisha miradi ya maendeleo, ambazo zinamtaka mwekezaji anayeanzisha mradi wa maendeleo apate kibali kutoka Mamlaka ya Mazingira.

"Mmeanzisha ujenzi wakati bado kuna taratibu hazijakamilika, hakuna tathmini yeyote ya kimazingira wala taarifa kutoka mamlaka inayosimamia mazingira, hii ni kinyume cha utaratibu... kwa vile nimekuja na Mkurugenzi husika, na kwa mamlaka aliyopewa, tunasitisha ujenzi mpaka mtakapokamilisha taratibu," alisema Mkuya.

Naye Mhandisi Idriss Nuooran kutoka Kampuni ya ZANTEXAS LIMITED, alikiri kutokamilisha taratibu za kimazingira, lakini alisema wameanza taratibu za kufanya tathmini ya kimazingira.

Sheha wa Shehiya ya Bweleo, Mataka Makame Mataka, alisema atahakikisha ujenzi wa kiwanda hicho hauendelei mpaka watakapotimiza taratibu za kisheria.

Naye Mkurugenzi wa ZEMA, Sheha Mjaja, alisema mwekezaji amekikuta kifungu cha 39(1) na ZEMA imetumia kifungu cha 23(1) (b) kusimamisha mradi huo na kumtaka afuate taratibu zilizopo za usajili wa miradi ya uwekezaji, ukodishwaji ardhi na tathmini ya mazingira.

"Kifungu cha 39 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ya mwaka 2015 kinasema ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya shughuli yoyote ambayo itakuwa na athari kubwa kwa mazingira na jamii bila ya cheti cha tathmini ya athari za kimazingira kinachotolewa na mamlaka kwa mujibu wa sheria hii," alisema.

Aliongeza: "Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki tathmini ya athari za kimazingira itafanywa kwenye hatua za mwanzo za mradi kabla haujaanza."

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**GODOWN NA YADI VINAHITAJIKA DAR KWA AJILI YA KUNUNUA**

Ukubwa wa eneo SQM 4,900 sawa na Ekari 1. Ofa ya kununua Bilioni 1. Piga Simu: 0628 336736 / 0686 302219

**TUNAUZA NA TUNANUNUA MAGODOWN NA YADI DAR**

Je unauza au unanunua Godown na Yadi Dar. Wasiliana na NJANI PROPERTY COMPANY. (NPC). Simu: 0628 336736/0686 302219

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**
**SHAURI LA MIRATHI NA. 41 YA 2021**
**Maombi ya barua ya Usimamizi wa Mirathi ya Marehemu**


**FRANCIS EMMANUEL KUZURURA……………………MAREHEMU**
**NA**
**EMMANUEL JOSEPH KUZURURA……………………MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 30 Mwezi wa 03 Mwaka 2021.

Hati hii imetolewa tarehe 10 Mwezi wa 03 Mwaka 2021.

## KUPOTEA KWA CHETI



**MAFURU EZEKIEL NDARO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0989-0055** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **KIBARA SEKONDARI** mwaka **2016.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **KBR/RB/464/2018.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HUSSEIN WAZIRI BURA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina **SUZUKI CARRY P/UP** yenye jina la **AHMED ISSA ABDUL** yenye namba za usajili **T 755 CHT. Chassis no. S110P01545.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/-DOD/RB/136093/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya Mwanzo MAKOLE**

**Usimamizi wa Mirathi No. 21/2021.**
**Ombi la SCOLASTICA SAMWEL MFILINGE kuteuliwa kuwa**
**Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu VICENT HOSEA MESHACK**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA**
**TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 22/3/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

## TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA GARI

**Nkondo Ngwininga Nkondo** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 827 AUQ** Fuso Mistubishi Injini namba ED 14606837. Kwa yeyote atakayeiona kadi hiyo ya gari awasiliane na Nkondo Ngwininga Nkondo kwa simu namba **0627476918** au atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilichopo karibu. **Rb namba Shy/TR/RB/193/2021.**

**NOTISI YA KUFUNGA KAMPUNI**
**A-Z CENTRE LIMITED**
**KAMPUNI NAMBA 95817**
**NOTISI YA MWEZI DESEMBA 2020**

MWENYEKITI ALIITISHA KIKAO KAMA ILIVYOSTAHILI NA WAHUSIKA WOTE WALIKUWEPO NA MKUTANO HUO ULIFANYIKA TAREHE 20 DESEMBA, MWAKA 2020, SAA 5:00 ASUBUHI NA MAKUBALIANO YAFUATAYO YALIFIKIWA:

WAHUSIKA WALIKUBALIANA KATIKA KIKAO HICHO KWA HIYARI YAO KUWA KAMPUNI HIYO IWE IMEFUNGWA TOKA TAREHE YA KIKAO 20/12/2020 NA HAKUTAKUWA NA BIASHARA YEYOTE AMBAZO ZITAKUWA ZINAENDESHWA KWA JINA AU KATIKA KAMPUNI.

KAMA MWANAHISA YEYOTE ATAKUWA NA LOLOTE JUU YA MAAMUZI HAYA ANATAKIWA AANDIKE BARUA YA KUPINGA MAAMUZI HAYA KWA MSAJILI WA MAKAMPUNI BRELA NDANI YA SIKU 21 KUTOKA TAREHE YA NOTISI HII.

HIVYO BASI MWENYEKITI ALITOA TAMKO KWAMBA HAKUTAKUWA NA BIASHARA YOYOTE ITAKAYOENDESHWA KATIKA KAMPUNI.

**MKUTANO ULIFUNGWA MNAMO SAA 8:30 MCHANA.**
**MAHALI: ARUSHA**
**Tarehe: 20/12/2020**

**ABDUL KARIM AHMAD DAKIK**
**Mwenyekiti wa Bodi**
**SRINIVASA RAO NALLURI**
**Sekretari wa Bodi**

**NOTISI YA KUFUNGA KAMPUNI**
**RELIANCE GROUP (T) LIMITED**
**KAMPUNI NAMBA 106465**
**NOTISI YA MWEZI FEBRUARY 2021**

MWENYEKITI ALIITISHA KIKAO KAMA ILIVYOSTAHILI NA WAHUSIKA WOTE WALIKUWEPO NA MKUTANO HUO ULIFANYIKA TAREHE 16th FEBRUARI, MWAKA 2021, SAA 5:00 ASUBUHI NA MAKUBALIANO YAFUATAYO YALIFIKIWA:

WAHUSIKA WALIKUBALIANA KATIKA KIKAO HICHO KWA HIYARI YAO KUWA KAMPUNI HIYO IWE IMEFUNGWA TOKA TAREHE YA KIKAO 16/2/2021 NA HAKUTAKUWA NA BIASHARA YEYOTE AMBAZO ZITAKUWA ZINAENDESHWA KWA JINA AU KATIKA KAMPUNI.

KAMA MWANAHISA AU MTU YEYOTE ATAKUWA NA LOLOTE JUU YA MAAMUZI HAYA ANATAKIWA AANDIKE BARUA YA KUPINGA MAAMUZI HAYA KWA MSAJILI WA MAKAMPUNI BRELA NDANI YA SIKU 21 KUTOKA TAREHE YA NOTISI HII.

HIVYO BASI MWENYEKITI ALITOA TAMKO KWAMBA HAKUTAKUWA NA BIASHARA YOYOTE ITAKAYOENDESHWA KATIKA KAMPUNI.

**MKUTANO ULIFUNGWA MNAMO SAA 9:30 MCHANA.**
**MAHALI: ARUSHA**
**Tarehe: 16/2/2021**

**ABDULKARIM AHMAD DAKIK**
**Mwenyekiti wa Bodi**
**WEMA MUNUO**
**Sekretari wa Bodi**

## KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**YOHANA MOSES MBISE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NO YA USAJILI **T 501 BTQ.** CHASSIS NO **KE7KE700009160.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **ARU/ARU/RB/134931/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NYUMBA (W)**
**ARUSHA-ARUSHA**

**MAOMBI NA. 164 YA MWAKA 2020**

**KISAKA INNOCENT MBAGA…………… MDAI**

**DHIDI YA**

**JOSEPH BROWN NGOO………MDAIWA WA KWANZA**

**AYUB ELIAS MAKOLO……………MDAIWA WA PILI**

**WITO /KUITWA SHAURINI**

**KWA: AYUB ELIAS MAKOLO……POPOTE ULIPO**

**KISAKA INNOCENT MBAGA**, amefungua shauri hili mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Arusha. Shauri husika limepangwa kutajwa mbele ya Mh.G.Kagaruki, Mwenyekiti tarehe 18/03/2021 saa tatu kamili asubuhi. Hivyo basi,unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili na pia utatakiwa kuhudhuria siku hiyo wewe au wakili wako au mtu yoyote atakayempa maelekezo juu ya shauri hili.

Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande moja na Hukumu kutolewa dhidi yako pasipo wewe kusikilizwa. Nakala ya maombi haya inapatikana katika Ofisi za Baraza zilizopo katika Jengo la Mkuu wa wilaya Arusha.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 18 mwezi Februari, mwaka 2021

MWENYEKITI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FRIDA FRANCIS BUBERWA** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T283DKB** aina ya **TOYOTA IST CHASIS** namba **NCP1100002876 ENGINE** namba **1NZC762993** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu. Polisi Taarifa **MWA/NYA/RB/137922/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**KIMARA, DAR ES SALAAM**
**MADAI NO. 18/2021**

**MDAI: EMMANUEL KAZUNGU**
**MDAIWA: DEBORA HIKWA**

Wewe **DEBORA HIKWA** popote ulipo unaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakamani mnamo **tarehe 1/3/2021** kama hautahudhuria basi Mahakama hii itasikiliza upande mmoja na uamuzi kutolewa.

## KUPOTEA KADI YA GARI

**ISSA KOMBO ISSA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye namba za usajili **T224 APN.** Yenye Chassis namba **LH71V0010361 na Engine namba LH7IV-002L-1929014.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. **Taarifa Polisi: TAN/RB/138975/2021.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.71/2021**

Ombi la **JOSEPH ANSELM MZAGA** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **ANSELM JOHN MKOBA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **Tarehe 12/04/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo . Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 10/03/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EDITHA COLMAN TARIMO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2849/0014** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **MASHATI SEKONDARI** mwaka **2018.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya Polisi: MOR/MOR/RB/15421/2021.**







OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji

THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Waziri Mkuu wa Ivory Coast, Rais zamani Somalia wafariki

**Abidjan,** IVORY COAST

WAZIRI Mkuu wa Ivory Coast, Hamed Bakayoko, amefariki dunia katika hospitali moja nchini Ujerumani, mamlaka zimesema.

Bakayoko, aliyekuwa akipata matibabu ya saratani, alifariki dunia jana, siku chache tu baada ya kuadhimisha siku yake ya kuzaliwa akifikisha miaka 56. Aliteuliwa kama Waziri Mkuu Julai, kufuatia kifo cha mtangulizi wake Amadou Gon Coulibaly.

Rais Alassane Ouattara alimwelezea Bakayoko kama kiongozi bora, mfano wa kuigwa kwa vijana na mwenye uaminifu usio kifani.

Bakayoko alipelekwa nchini Ufaransa Februari, mwaka huu, kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu na baadaye akahamishwa Ujerumani kwa sababu afya yake ilikuwa inaendelea kuzorota.

**Rais Mohamed Abdullahi Farmajo, aliagiza bendera zote nchini kupeperushwa nusu mlingoti kwa siku tatu, kwa heshima ya rais huyo wa zamani.**

Waziri mkuu huyo ambaye alikuwa mkurugenzi mtendaji wa vyombo vya habari, alitekeleza jukumu kubwa katika maridhiano nchini Ivory Coast wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe kipindi cha muongo wa kwanza wa karne.

"Alikuwa mshikadau mkuu katika siasa na maridhiano," alisema Msemaji wa upinzani wa Chama cha Ivorian Popular Front, Issiaka Sangare, katika Shirika la Habari la AFP.

Mbali na jukumu lake kama waziri mkuu, Bakayoko pia alikuwa waziri wa ulinzi nchini humo.


Patrick Achi aliteuliwa kama waziri mkuu wa muda huku Tene Birahima Ouattara, kaka mdogo wa rais, akitajwa kama waziri wa ulinzi wa muda.

Wakati huohuo, BBC ilisema Rais wa zamani wa Somalia, Ali Mahdi Mohamed, amefariki usiku jana katika hospitali moja nchi jirani ya Kenya akiwa na umri wa miaka 82.

Alingia madarakani mwaka 1991 baada ya Rais Siad Barre kung'olewa madarakani na kusalia madarakani hadi mwaka 2000. Nafasi yake baadaye ilichukuliwa na Abdiqasim Salad Hassan.

Rais Mohamed Abdullahi Farmajo, aliagiza bendera zote nchini kupeperushwa nusu mlingoti kwa siku tatu, kwa heshima ya rais huyo wa zamani.

Kamati ya kitaifa ya mazishi imeteuliwa huku wanasiasa na maofisa wa zamani wa serikali wakituma risala za rambirambi. **RFI/BBC**




Mfalme Naruhito wa Japan (kulia) na Masako Owada wakiinama mbele ya madhabahu iliyojengwa kama kumbukumbu ya waathirika wa Tsunami na tetemeko la ardhi la Machi 11, mwaka 2011, kwenye ibada ya kitaifa jijini Tokyo, jana. Ikiwa ni miaka 10 tangu kutokea tukio hilo lililosababisha vifo takribani 18,000. **PICHA:AP**

# Afungwa siku moja kumuua mumewe

**Nairobi,** KENYA

MAHAKAMA nchini Kenya imemhukumu kifungo cha siku moja mwanamke aliyemuua mume wake, mwaka mmoja uliopita, kwa mujibu wa gazeti la Daily Nation.

Jaji Roselyn Aburili alimkuta Truphena Ndong'a Aswani na kosa la kumuua mumewe Desemba 14, mwaka jana.

"Hakuwa na sauti. Alinyamazishwa kwa kichapo hadi akakubali kupigwa ni jambo la kawaida. Ana bahati yuko hai," gazeti hilo lilinukuu maneno aliyotumia Jaji Aburuli.

Mtuhumiwa alionewa huruma na Jaji kwa kuvumilia mateso na kumhukumu kifungo cha siku moja ambacho hakikujumuisha kuzuiliwa ndani.

Jaji Aburili aliagiza idara ya mahakama kuhakikisha Truphena amepewa usafiri wa kwenda hadi nyumbani kwake Ukwala katika Kaunti ya Siaya Magharibi mwa Kenya.

Truphena (49) aliifahamisha mahakama kwamba alivumilia mateso katika ndoa yake, ili kumtunza mwanawe wa kiume na watoto wengine wanne walioachwa na wake wenzie wa awali.

Mahakama ilifahamishwa kuwa mumewe, James Obochi alirejea nyumbani usiku akiwa mlevi kama ilivyo ada akapewa chakula.

Baada ya kula huku akiwa amelewa alianza kuzozana na mkewe akidai kupewa hati miliki ya shamba la familia na alipokataa kumpatia nyaraka hizo kwa kuhofia anaweza kuzitumia kuuza shamba lao, alikimbilia chumbani na kuchukua panga kumkata mke wake.

Truphena, alimshinda nguvu mumewe katika purukushani hiyo, akamuua katika juhudi za kujilinda. **BBC**

## Dunia yakumbuka mwaka 1 corona ikitangazwa janga

**New York,** MAREKANI

WAKATI dunia ikikumbuka mwaka mmoja tangu virusi vya corona vilipotangazwa kuwa janga na chanjo kuanza kutolewa, maisha bado hayajarudi kama kawaida kutokana na vikwazo mbalimbali vilivyowekwa ili kuzuia kusambaa kwa ugonjwa wa COVID-19.

Machi 11, mwaka jana, inatajwa kuwa kumbukumbu ya dunia baada ya Shirika la Afya Duniani (WHO), lilipoutangaza rasmi ugonjwa wa COVID-19.

"Tumeingiwa na wasiwasi juu ya ongezeko la maambukizi ya virusi vya corona na kiwango duni cha kutochukua hatua. Kwa hiyo tumefanya tathmini yetu na tumeamua kuutangaza ugonjwa wa Covid-19 kuwa janga la dunia," alisema Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Tedros Ghebreyesus.

Corona haikuathiri sekta ya afya pekee, bali iliyumbusisha uchumi wa dunia.

Janga hilo liliisimamisha dunia, hususan kwenye usafiri wa anga ukazuiwa, serikali mbalimbali zikaweka vikwazo ikiwamo kuwazuiwa watu kusafiri au kutotoka nje kwa muda fulani na hata kupiga marufuku shughuli za kiuchumi na masomo.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la AFP, zaidi ya dozi milioni 300 zimesambazwa kwa karibu nchi 140 duniani. **DW**

## Waasi DRC, Msumbiji wahusishwa na IS

**Kinshasa,** DRC

MAREKANI inasema makundi ya waasi Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na nchini Msumbiji ni magaidi kutoka nje ya nchi hizo.

Nchini DRC, kundi la ADF limetajwa kuwa la kigaidi huku Al Ansar al-Sunna, linalofahamika kama Al-Shabaab nchini Msumbiji, yakitajwa kushirikiana na kundi la kijihadi la Islamic State (IS).

Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, ilisema viongozi wa makundi hayo, wanashirikiana kwa karibu na wale wa Islamic State na sasa wamekewa vikwazo.

Kundi la ADF limeendelea kusababisha ukosefu wa usalama Mashariki mwa DRC hasa katika Wilaya ya Beni na tangu kuanza kwa mwaka 2021, limesababisha vifo vya mamia ya raia.

Pia kundi la Ansar al-Sunna, limetekeleza mauaji ya zaidi ya watu 1,300 nchini Msumbiji tangu Oktoba mwaka 2017. **BBC**

# HAKIMI KUMRITHI BELLERIN ARSENAL



**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal imeingia kwenye rada za kumsajili beki wa kulia wa Inter Milan, Hakimi Achraf wakitaka kutumia uchochoro wa mgogoro unaoikumba klabu hiyo.

Kwa mujibu wa gazeti la Telegraph, Arsenal wanataka kumsajili beki huyo wa Inter Milan, Hakimi kama mbadala wa Hector Bellerin, ambaye ametajwa kuwa yuko nje ya London msimu huu wa joto.

Hakimi mwenye umri wa miaka 22, ni mdogo kwa miaka mitatu kuliko Bellerin na anacheza kwa kiwango cha juu sana nchini Italia, akifunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho nne kwenye Serie A msimu huu.

Uwezo wake wa kushambulia ungewapa washikabunduki hao chaguzi kadhaa za jinsi ya kumpeleka, ingawa Bellerin akiondoka, angeweza kuanza katika kampeni ijayo ya ulinzi.

# Simeone aweka rekodi Atletico Madrid

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone ameipita rekodi ya Luis Aragones ya kushinda mechi nyingi ndani ya Atletico Madrid kama kocha mkuu.

Kocha huyo raia wa Argentina alifikisha ushindi wa 309 siku ya Jumatano kwa ushindi wa 2-1 dhidi ya Athletic Bilbao, matokeo yaliyoipeleka timu hiyo katika nafasi ya kwanza kwa tofauti ya alama sita mbele ya Barcelona na Real Madrid kwenye msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Iker Munian aliipa Athletic Bilbao goli la kuongoza katika dimba la Wanda Metropolitano, lakini Marcos Rlorente alisawazisha mwishoni mwa kipindi cha kwanza na Luis Suarez alifunga bao la pili kwa mkwaju wa penalti mapema kipindi cha pili.

Ushindi huo wa Simeone umepatikana katika mechi yake ya 514 akiwa kama kocha.

Aragones mtu pekee aliyeiongoza Atletico kwenye michezo mingi alifikisha ushindi wa 308 katika mechi 612.

Atletico imeenda sare mara 121 na kupoteza 84 wakiwa chini ya Simeone, ambaye alichukua mikoba ya kuinoa timu hiyo mwaka 2011 na amekuwa kocha wao mwenye mafanikio wa muda wote.





# Pele kupewa Maracana

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

UWANJA wa Taifa wa Brazil wa Maracana utabadilishwa jina ambapo utapewa jina la mchezaji nguli wa soka nchini humo, Edson Arantes do Nascimento maarufu kama Pele.

Hii ni baada ya kura za maoni ya kubadili jina hilo zilizopigwa na baraza la mji wa Rio de Janeiro kupitisha mabadiliko hayo na sasa ni suala la Gavana kuidhinisha pendekezo hili kabla ya kurasimisha matumizi ya jina hilo.

Pele akiwa na makombe matatu ya Kombe la Dunia aliyobeba wakati akiwa mchezaji wa Timu ya Taifa ya Brazil.

Mabadiliko haya yatabadili jina la Maracana na kuwa Uwanja wa Edson Arantes do Nascimento Rei Pele. Neno 'Rei' lina maana ya Mfalme (kwa lugha ya Kireno)

Pele anatambulika kama mchezaji bora wa muda wote nchini Brazil.

Hii ni baada ya kutwaa makombe matatu ya dunia, pia, mwaka 1969 alifunga goli lake la 1000 katika uwanja huo wakati alipokuwa akiitumikia Santos kwenye mchezo dhidi ya Vasco da Gama.

Takribani watu 200,000 walikuwapo uwanjani hapo kushuhudia Uruguay ikiifunga Brazil kwenye fainali ya Kombe la Dunia mwaka 1950 na sasa uwanja huo umeripotiwa kuwa na uwezo wa kuhimili mashabiki 78,838 tu.

HABARI MICHEZO

# Klopp akataa kuiongoza Ujerumani

**LIVERPOOL,** England

BAADA ya kocha wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Joachim Low kutangaza kuachia ngazi baada ya mashindano ya mataifa ya Ulaya, kocha wa Liverpool Jurgen Klopp ajiweka mbali na nafasi hiyo.

Jina la Klopp lilitajwa kama mrithi sahihi wa Low na pengine wengi wanadhani ni muda sahihi kwake kukinoa kikosi cha timu ya taifa lake baada ya kuvinoa vikosi vya Mainz, Dortmund na sasa Liverpool.

Baada ya kubeba taji la Uefa (2019) na Ligi Kuu England (2019/20), Liverpool wanahaha msimu huu wakiwa nafasi ya nane ikiwa ni pointi saba pungufu ili kuingia kwenye nafasi ya nne bora.

Alipoulizwa na waandishi wa habari kuhusu kutajwa kwake huko, Klopp alijibu, "Kwamba ninapatikana kwenye kazi baada ya msimu huu? Hapana.

"Mtu mwingine ataifanya kazi hiyo, kwa namba ya makocha wengi wazuri wa Ujerumani.

"Nina uhakika Shirikisho la Soka la Ujerumani litapata suluhisho sahihi kwenye nafasi hiyo.

"Bado nimebakiza miaka mitatu kwenye mkataba wangu na Liverpool. Ni rahisi, unasaini mkataba na unausimamia. Nimeisimamia mikataba yangu yote nilipokuwa Mainz na Borussia Dortmund."





# BALLACK ATAKA WERNER KUPEWA MUDA

**MUNICH,** Ujerumani

KIUNGO wa zamani wa Chelsea, Michael Ballack ameungana na kocha wa timu hiyo, Thomas Tuchel juu ya kumpa muda zaidi mshambuliaji, Timo Werner ili aweze kuonyesha makali yake.

Werner mwenye umri wa miaka 24 kiwango chake kimeporomoka na amekuwa akipambana kuboresha kiwango chake tangu kuja kwake hapo akitoka Leipzig.

Kitu kilichopelekea mashabiki wa Blues hao kumpigia kelele kuwa hana hadhi ya kuchezea klabu hiyo kitu kilichompelekea Tuchel kumkingia kifua, akiwataka wavute subira kwani mambo makubwa yanakuja kutoka kwake na kuungwa mkono na Ballack.

Ballack akizungumza na gazeti la Bild amesema kwamba, Werner anatakiwa kupewa muda wa kutosha ili kuonyesha kiwango chake.

"Naamini ni wakati muafaka sasa Werner kupewa nafasi ya kutosha, nina imani kubwa kwake," alisema Ballack.

Aliongeza: "Kuna wakati mchezaji huwa anapitia kwenye wakati mgumu, hivyo nina imani kubwa kwamba atarudi kwenye kiwango chake."

# *Fletcher mkurugenzi mpya United*

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imefanya mabadiliko kwa kumchagua John Murtough kuwa mkurugenzi wa soka wa kwanza kwenye klabu hiyo na kiungo wa zamani Darren Fletcher akichaguliwa kuwa mkurugenzi wa ufundi.

Makamu Mwenyekiti Mtendaji, Ed Woodward alisema: "Huu ni uteuzi mkubwa kabisa kwa ajili ya kuchochea maendeleo ambayo tumekuwa tukipiga katika miaka ya karibu ili kufikia mafanikio.

"Tumeshatafuta namna ya kuendesha mipango yetu ya soka na faida yake inaonekana kwa kuona wachezaji makinda waliopo kwenye akademi wanakuja na kucheza timu za wakubwa na tunataka kuboresha idara yetu ya usajili pia.

"John amekuwa mtu muhimu katika maendeleo yetu kwenye maeneo hayo na amekuwa na uelewa mkubwa katika kuhakikisha klabu inaendelea na utamaduni wake wa kupandisha wachezaji vijana kutoka kwenye akademi ili kuendeleza timu za wakubwa.

Woodward sasa atajiweka pembeni katika uhusika wake wa moja kwa moja kwenye usajili na hivyo kuwekeza nguvu kwenye majukumu mengine ya kuendesha klabu.

Kwa muda mrefu, United ilikuwa ikihusishwa na mpango wa kumchukua mmoja wa wachezaji wake wa zamani kwenda kuwa mkurugenzi wa soka, akiwamo Edwin van der Saar, ambaye ana cheo kama hicho huko Ajax.

Klabu ilitaka kufanya uteuzi huo tangu kocha akiwa Jose Mourinho, lakini Mreno huyo aliweka pingamizi.

Murtough mwanzoni alikuwa akishikilia cheo cha kuwa mkuu wa maendeleo ya soka na amekuwa United kwa miaka saba, tangu alipotua hapo wakati wa David Moyes.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HATIMA YA RONALDO JUVENTUS SHAKANI

Ni kutokana na mshambuliaji huyo kushindwa kuisaidia klabu hiyo kufanya vyema...

**TURIN,** Italia

BAADA ya Juventus kuondolewa kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kumeibuka taharuki kuhusu hatima ya Cristiano Ronaldo na kocha Andre Pirlo.

**Huu ni mwendelezo wa matokeo mabaya ya Juventus baada ya kukamilisha usajili wa Ronaldo kwa ada ya pauni milioni 85 misimu miwili iliyopita.**

Juventus imeondolewa katika mashindano hayo ikiwa ni msimu wa tatu mfululizo haijafika hatua ya nusu fainali.

Juve walijikuta wakiangukia pua kwenye mikono ya Ajax katika hatua ya robo fainali msimu wa 2018/19 kabla ya kuadhibiwa na Lyon msimu wa 2019/2020, kisha msimu huu wakapoteza dhidi ya FC Porto.

Kiuhalisia usajili wa Ronaldo ulilenga zaidi kuisaidia Juve kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini hali imekuwa tofauti sana. Itakumbukwa msimu uliopita, Juve walimfukuza kazi kocha wao Maurizio Sarri baada ya kushindwa kufanya vizuri kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya licha ya kubeba taji la Serie A.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Ufundi wa klabu hiyo, Fabio Paratici amesafisha hali ya hewa kwa kusema kuwa, "bado kuna mwaka mmoja kwenye mkataba wa Ronaldo hadi Juni 2022".

"Kuongeza mkataba wa Cristiano Ronaldo sio kipaumbele kwa sasa, bado kuna muda wa kulizungumzia hilo," alisema Paratici akinukuliwa na Sky Sport.

Juventus bado wanakibarua cha kutetea ubingwa wao wa Serie A msimu huu wakiwa wamezidiwa pointi 10 na vinara wa ligi hiyo, Inter Milan.

## ZISIKUPITE

### AGUERO ANUKIA BARCA

BARCELONA imempa ofa ya mkataba mshambuliaji wa Argentina, Sergio Aguero, 32, ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu pale Manchester City. ***(Tycsports)***

### WERNER KUWEKWA SOKONI

CHELSEA inaweza kumuuza straika wa Ujerumani, Timo Werner kipindi cha majira ya joto baada ya kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 25 kwa pauni milioni 54 kutoka RB Leipzig. ***(Football Insider)***

### ALABA BADO SANA

WAKALA wa mlinzi wa Austria, David Alaba amekanusha madai ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 ambaye mkataba wake unamalizika msimu huu pale Bayern Munich, amekubali kujiunga na Barcelona. ***(Goal)***

### CAVANI AVUTA SUBIRA

STRAIKA wa Manchester United, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 34, atasubiri hadi mwishoni mwa msimu huu kabla ya kuamua hatima yake. ***(ESPN)***

### JUVE YAFUNGUKA

KUONGEZWA mkataba mpya kwa Cristiano Ronaldo "sio kipaumbele kwa sasa" kwa Juventus, amesema Mkurugenzi wa soka wa klabu hiyo, Fabio Paratici. ***(Express via Sky Italia)***

### MADRID KUMUUZA VARANE

REAL Madrid itasikiliza ofa kwa mlinzi wake, Raphael Varane, 27, kipindi hiki cha majira ya joto. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa inaaminika anataka kwenda kucheza Ligi Kuu England. ***(AS)***

### GABRIEL AWINDWA

LIVERPOOL inamkodolea macho winga kinda wa Santos, Angelo Gabriel mwenye umri wa miaka 16 ambaye ni raia wa Brazil. ***(Sport Witness)***

### NEWCASTLE SOKONI

NEWCASTLE inapanga kumsajili mlinzi wa pembeni, Matthew Bondswell, 18, kutoka RB Leipzig. ***(Telegraph)***

### EDER ANUKIA EPL

MSHAMBULIAJI wa Ureno, Eder anawaniwa na Brighton,33, huku mchezaji huyo akipanga kuondoka Lokomotiv Moscow kipindi cha majira ya joto. ***(A Bola)***

### DERBY KUUZWA

MFANYABISHARA wa Hispania, Erik Alonso amefikia makubaliano ya kuinunua klabu ya Derby ya England. ***(Athletic)***

### RANGNICK KUMRITHI LOW

KOCHA wa zamani wa RB Leipzig, Ralf Rangnick amesema anapenda kuchukua nafasi ya Joachim Low kama kocha wa timu ya taifa ya Ujerumani. ***(Sky Sports)***

## Namungo yarejea leo na mikakati

**Na Shufaa Lyimo**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Namungo Fc wanatarajiwa kurejea nchini leo huku wakijipanga 'kupindua meza' katika mchezo wa marudiano wa michuano hiyo.

Namungo ikiwa ugenini Morocco, ilikubali kichapo cha bao 1-0 katika mchezo wake wa kwanza wa hatua ya makundi dhidi ya wenyeji Raja Casablanca.

Mwenyekiti wa Namungo, Hassan Zidadu, alisema wachezaji wote wapo salama na wanatarajia kuwasili nchini leo saa saba mchana na wanawashukuru wenyeji wao kwa ukarimu waliowapatia wakati wote.

Zidadu alisema wachezaji wote baada ya mchezo wa juzi wanaendelea vizuri na hakuna taarifa za kupatikana kwa mtu yoyote kuwa na ugonjwa wa corona.

"Ninawapongeza wachezaji wetu kwa kupambana, ukizingatia ni wageni katika mashindano hayo, lakini wameonyesha uwezo mkubwa, kikubwa tunaendelea kufanya mipango ya kuhakikisha tunasonga mbele kwa kuiwakilisha vizuri bendera ya Taifa," alisema Zidadu.

## Mchangani yalia ukata unaimaliza

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UKOSEFU wa fedha ndio sababu kubwa ya kikosi cha Mchangani United kupata matokeo mabaya katika Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mchangani United, Seif Bausi alisema timu yake haina fedha za kujiendesha na hivyo imekuwa na wakati mgumu katika kukamilisha programu zake.

Bausi alisema tangu kuanza kwa msimu huu timu hiyo imekosa fedha za kuendesha programu mbalimbali ikiwamo kulipa posho za wachezaji katika siku za mechi pamoja na kukamilisha mchakato wa kusajili wachezaji imara wakati wa dirisha dogo.

Kiongozi huyo amewaomba wakazi wa Mchangani United kujitolea kuisaidia timu hiyo ili ifanye vizuri katika kipindi hiki ambacho ligi inapambana kujinusuru na janga la kushuka daraja.

Mchangani United imepokea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Mchangani FC katika mechi ya Ligi Daraja la Kwanza iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Mau A wakati Uhamiaji imetoka kifua mbele kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mwembe Makumbi City huku New King ikichapwa magoli 2-0 na Dulla Boys.

# KOCHA PRISONS AJIITA MOURINHO WA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya timu yake kutoka sare na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Prisons, Shaaban Kazumba, ametamba yeye ndiye Mourinho wa Tanzania kutokana na kuitengeneza vyema safu yake ya ulinzi kwa kuwa ngumu kupitika na kufungika kirahisi.

Kazumba alisema baadhi ya watu wamekuwa wakimfananisha na kocha huyo wa Tottenham Hotspur ya England, Jose Mourinho kutokana na mfumo wake wa ufundishaji kwa kutengeneza safi ngumu ya ulinzi na kwa sasa amelikubali na watu wameona shughuli yake.

**Kocha huyo alisema mfumo alioutengeneza ulisababisha wasionekane kama wako pungufu na kuipa wakati mgumu Simba na hiyo ndiyo aina yake ya ufundishaji na hajali kama watu watasemaje.**

"Mwamuzi amechezesha vizuri, labda kidogo nina wasiwasi na ile kadi nyekundu. Simba ni timu nzuri na inatuwakilisha kimataifa, kwa hiyo tulikuja kwa kuiheshimu na tulijua mechi itakuwa ngumu tu," Kazumba alisema.

Kwa matokeo hayo, Simba imeshindwa kuifunga Prisons kwa misimu miwili, tangu ilipopata ushindi Mei 5, 2019 kwa bao la Emmanuel Okwi kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, Simba ikishinda goli 1-0, msimu wa 2018/19.

Msimu wa 2019/20, timu hizo zilitoka suluhu kwenye mechi zote, Novemba 7, 2019, Uwanja wa Uhuru na Juni 28, 2020 kwenye Uwanja wa Sokoine.

Msimu huu, Simba ilichapwa bao 1-0, mjini Sumbawanga, Oktoba 22, mwaka jana, kabla ya sare ya bao 1-1 juzi.

Maafande hao tayari wameanza kutamba kuiondoa Yanga katika mechi ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa mapema mwezi ujao kwenye Uwanja wa Nelson Mandela.




Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya KCB, Christine Manyenye (wapili kulia), akikabidhi mfano wa hundi kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Jackson Group, Kelvin Twissa (wapili kushoto) kwa ajili ya kudhamini pambano la ubingwa wa Afrika katika uzito wa Superweltwer litakalofanyika Machi 26, mwaka huu, jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mwakilishi wa DStv, Baraka Shelukindo na Mkurugenzi Mtendaji wa Plus Tv, Ramadhani Bukini. **MPIGAPICHA WETU**

# *Mwakinyo ulingoni, KCB yajitosa*

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA Hassan Mwakinyo anatarajia kupanda ulingoni kuwania ubingwa wa Afrika (ABU) wa uzito wa Superwelter dhidi ya Mzimbabwe Brendon Denes katika pambano litakalofanyika Machi 26, mwaka huu, kwenye Ukumbi wa Next Door Arena jijini Dar es Salaam.

Katika kufanikisha pambano hilo la raundi 12, benki ya KCB imetangaza kutoa kiasi cha Sh. milioni 94.4.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Jackson Group Sports, Kelvin Twissa alisema jana mkanda huo kwa sasa upo wazi na wameamua kumwandalia Mwakinyo pambano ili kumwezesha kuingia katika orodha ya viwango vya shirikisho maarufu la ngumi za kulipwa duniani za WBC.

Twissa alisema siku hiyo kutakuwa na mapambano mengine ya utangulizi ambapo Jongo Jongo naye atawania ubingwa wa ABU dhidi ya Olanrewaju Durodora wa Nigeria huku Ibrahim Class atapanda ulingoni dhidi ya bondia atakayetangazwa baadaye.

Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa KCB, Christine Manyenye alisema wameamua kutoa kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya pambano hilo ili kuendeleza mchango wao katika maendeleo ya michezo nchini.


Manyenye alisema benki yao pia inadhamini Ligi Kuu Bara, mashindano ya Ndondo Cup na riadha ya Rock City Marathon.

"Ni faraja kubwa kwetu kujihusisha na maendeleo ya michezo nchini ikiwa pamoja na jamii, hivyo tunatarajia mashabiki wa ngumi za kulipwa watajitokeza kwa wingi siku hiyo na mabondia wa Tanzania watashinda," alisema Manyenye.

Naye Mkuu wa Masoko wa Multichoice Tanzania, Baraka Shelukindo, alisema pambano hilo linatarajia kuonekana zaidi ya nchi 30 barani Afrika.

# Michezo

Ijumaa Machi 12, 2021
Nipashe




Hatima ya Ronaldo Juve shakani UKURASA 22




Mshambuliaji wa Simba, Bernard Morrison (kulia), akijiandaa kumtoka mchezaji wa Tanzania Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga yajitabiria mambo mazuri

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kutangaza kumrejesha Kocha, Juma Mwambusi katika kikosi chake, mabosi wa Yanga wametamba timu yao itarejea katika ushindani wa kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu wa 2020/21.

Yanga yenye pointi 50, ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakifuatiwa na watani zao, Simba yenye pointi 46, lakini wamecheza mechi pungufu tatu.

Mwenyekiti wa Yanga, Mshindo Msolla, aliliambia gazeti hili uongozi wake umefikia uamuzi wa kumkabidhi mikoba Mwambusi kwa sababu kocha huyo anaifahamu vyema timu na kwa muda uliopo, anaweza kurekebisha mapungufu na kurejea kwenye makali yake.

Msolla alisema Yanga ina uwezo wa kukabiliana na ushindani uliopo katika ligi na hatimaye kutimiza malengo waliyonayo kwenye msimu huu.

"Hatujapotea katika ushindani, muda wa kujiimarisha upo, tunaamini bado tuko katika mbio za ubingwa, kikubwa ni kuendelea kupambana ili kufikia malengo, tutaimarisha mipango na mikakati iliyopo," Msolla alisema.

Mwambusi amerejesha katika kikosi hicho baada ya mabosi kutangaza kuachana na aliyekuwa kocha mkuu, Cedric Kaze pamoja na benchi zima la ufundi.

# Simba: Bado tuko vitani

## Kocha afunguka Prisons imewapunguza kasi, shabiki afariki Namtumbo...

**Saada Akida na Stevie Chindiye,**

NAMTUMBO

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes amewatetea wachezaji wake baada ya kulazimisha sare, shabiki wa timu hiyo, Ally Kuntika (71), amefariki dunia baada ya kudondoka ghafla kufuatia straika, Chris Mugalu kukosa penalti katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Tanzania Prisons iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi.

**Gomes aliliambia gazeti hili mara nyingi amekuwa akifanyia mazoezi upigaji wa penalti, lakini anaamini suala la kukosa pigo hilo liko katika sehemu ya mchezo hivyo hataweza kuwalaumu wachezaji wake endapo watashindwa kufunga.**

"Ni kweli tumekosa penalti tatu katika michezo mitatu tofauti, hili sio jambo la kuwalaumu wachezaji wangu kwa kushindwa kupiga penalti pamoja na free kick, ingawa tunafanyia kazi mazoezini katika kipengele hicho, yote hayo yanatokana na mpira, wachezaji wamecheza vizuri ila bahati haikuwa upande wetu," alisema Gomes.

Kocha huyo aliongeza hakufurahishwa na matokeo hayo kwa sababu iko nje ya mipango yao ya kuhitaji pointi tatu muhimu ili kujiweka katika mazingira mazuri kwenye msimamo wa ligi hiyo na katika mbio za kuwania ubingwa.

"Mipango ilikuwa kupata pointi tatu, lakini tumepata pointi moja, niwapongeze wachezaji wangu kwa kujitoa na kupambana, sasa tunaenda kufanyia kazi mapungufu yetu, niwapongeze wapinzani wetu kwa kuingia uwanjani kwa mbinu ya kuzuia hali ambayo wamefanikiwa," alisema Gomes.

Naye Kocha Mkuu wa Tanzania Prisons, Shaaban Kazumba, aliwapaongeza wachezaji wake kwa kufanya vyema majukumu aliyowapa mazoezini na kufanikiwa kupata pointi moja dhidi ya mabingwa hao watetezi wa ligi hiyo.

Kazumba alisema wachezaji wake walifanikiwa kufuata mbinu alizowaelekeza kwa kuwazuia Simba kufunga kwa kutowapa nafasi ya kuwashambulia kama ilivyo kawaida yao.

Alisema anaifahamu Simba inavyocheza mpira wake na yeye alihakikisha kikosi chake kinacheza kwa tahadhari na kuwaheshimu wapinzani wao kwa kutumia mfumo wa 'kupaki basi'.

"Tumefanikiwa kuingia na mbinu hiyo, Simba ni timu nzuri na tunajua imetoka kumfunga Al Ahly hivi karibuni, hivyo sikuangalia hilo na baada ya mapumziko niliwaambia wachezaji wangu wasiende ovyo, pia niwapongeze wapinzani wangu kwa kupambana na kupata bao la kusawazisha," alisema Kazumba.

Baada ya mchezo huo, Simba inatarajia kuendelea na mazoezi leo kwa ajili ya kuwakaribisha El Merrikh kutoka Sudan katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa Machi 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Namtumbo, Geofrey Kalikawe alisema katika taarifa yake marehemu Kuntika alikutwa na umauti akiwa katika 'kibanda umiza' akiwa anaangalia mechi hiyo, alionekana kuwa na furaha kubwa wakati timu yake ilipopata penalti hiyo.

Kalikawe aliendelea kueleza kuwa marehemu alikaa katika benchi akiwa na watazamaji wengine wakati wanasubiri mchezaji wa Simba kupiga mpira wa penalti dhidi ya timu ya Tanzania Prison palikuwa na mabishano ya hapa na pale wengine wakidai anakosa na yeye akidai hawezi kukosa.

Alisema kitendo cha Mugalu kukosa penalti kilimuumiza na kumfanya ainame na baada ya muda mfupi mashabiki wenzake walibaini amefariki kwa sababu ya kushindwa kuwapa ushirikiano.

Mtoto wa marehemu, Barakati Kuntika alisema baba yake alikuwa ni shabiki mkubwa wa Simba na alishawahi kutoa zawadi ya mbuzi na kuikabidhi timu ilipokuwa inapita Namtumbo ikielekea Songea kucheza dhidi ya Majimaji.

Alisema marehemu ambaye ameacha wake watatu na watoto 17, atazikwa katika makaburi ya Namtumbo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >